epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Machi 13, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

UKURASA 5

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581614
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

## NYOTA MAN UNITED FITI KUIKABILI LIVERPOOL

# Upasuaji waokoa mtoto asiyemeza chakula miaka 6

UKURASA 2



**Mama** aliyeua wanawe wawili kwa soda yenye sumu naye afa kwa sumu UK.4

MIAKA 3 YA SAMIA

**Aenda** na staili ya vitendo kuliko maneno mengi UK.3



**Waandishi** waachia nyumba ya Mbowe, wabaki na mil. 62/-



UK.5



Jopo la wataalamu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) lililomfanyia upasuaji kwa njia ya matundu madogo mtoto aliyekuwa na tatizo la kumeza chakula kwa miaka sita. **Picha ndogo:** Sehemu ya koo wakati wa upasuaji huo. **PICHA: MNH**

## Nyumba ya wakili yabomolewa kutoa haki ardhi ya mjane

UKURASA 4

## Mtaalamu wa Hisabati afukua mzizi wa kufeli kusikoisha

UKURASA 2

**MICHEZO** **MANDONGA AJA NA 'JIWE LA MOTO'** UK.23

**KATUNI** UK.6

# Upasuaji waokoa maisha mtoto asiyemeza chakula miaka sita

**Na Christina Mwakangale**

MTOTO aliyeshindwa kumeza chakula kwa miaka sita kutokana na koo lake kuziba, amefanyiwa upasuaji katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na kuokoa maisha yake.

Maradhi hayo ambayo matabibu wameyabatiza jina la taalamu yao la Achalasia Cardia, yametibiwa katika hospitali hiyo ya hadhi ya juu zaidi nchini, madaktari wakimfanyia upasuaji kwa njia ya tundu dogo (Laparoscopic Hellers Myotomy).

Kwa mujibu wa uongozi wa MNH, mtoto huyo mwenye umri wa miaka saba, alikumbwa na maradhi hayo akiwa na umri wa mwaka mmoja. Bingwa Mbobezi wa Upasuaji Mfumo wa Chakula, Ini na Mbobezi wa Upasuaji wa Matundu Madogo MNH, alisema jana kuwa upasuaji huo ulifanywa hospitalini huko mwishoni mwa wiki iliyopita.

Dk. Kitembo Kibwana alisema matibabu hayo yamefanywa baada ya mtoto huyo kuishi na tatizo hilo kwa miaka sita, upasuaji ukichukua saa moja na nusu.

Akifafanua kuhusu ugonjwa huo, bingwa huyo alisema mtoto huyo alishindwa kumeza chakula kutokana na mishipa yake ya fahamu ya koo la chakula kuharibika na kushindwa kumeza kirahisi.

Bingwa huyo aliyeongoza jopo la wataalamu wenzake katika matibabu hayo, alisema upasuaji huo ulipunguza kizuizi kati ya umio (koo la chakula) na tumbo na kugawanya safu ya misuli kutoka kwenye umio hadi kwenye tumbo ili kumwezesha mtoto huyo kumeza chakula kwa urahisi.

"Achalasia ni ugonjwa ambao hufanya iwe vigumu kwa chakula na kioevu kupita kutoka koo la kumeza linalounganisha kinywa na tumbo (umio) ndani ya tumbo.

"Tatizo hili hutokana na mishipa kwenye umio kuharibiwa na mwili wenyewe (auto-immune) au baadhi ya maambukizi na kusababisha umio kupooza na kupanuka kwa muda na hatimaye kupoteza uwezo wa kukamua chakula hadi tumboni,

"Matokeo yake, chakula hicho hujikusanya kwenye umio, wakati mwingine huchacha na kurudishwa hadi mdomoni kikiwa na ladha yenye uchungu," alifafanua.

Bingwa huyo aliendelea kufafanua, akisema: "Wananchi wenye changamoto ya kumeza wafike hospitalini, ili kufanyiwa uchunguzi na kisha kupatiwa matibabu stahiki.

"Huduma hii hutolewa kwa muda mfupi na kumruhusu mgonjwa ndani ya siku mbili kwenda nyumbani kuendelea na shughuli zake."

Alibainisha kuwa tayari hospitali hiyo imefanya upasuaji wa aina hiyo kupitia njia ya matundu (laparoscopy) kwa wagonjwa 24 kwa ufanisi mkubwa. Kati yao, watatu ni watoto.



Mufti Mkuu wa Tanzania, Dk. Abubakari Zubeir, akizungumza wakati wa dua ya kitaifa ya kumwombea Rais mstaafu Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi, Makao Makuu ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Kinondoni, Dar as Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# 'Acheni dhana ya uchuro katika bima na pensheni'

**Na Christina Mwakangale**

KUKATA bima na kuwekeza katika mifuko ya hifadhi kijamii si uchuro bali ni mfumo uliowekwa ili kutoa msaada wakati wa matukio ya ghafla kama vile ajali na ugonjwa.

Mtafiti kutoka Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Tanzania (FSDT), Nellin Njovu, alitoa kauli hiyo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano uliolenga kupata mbinu za kutatua matatizo yanayokabili jamii na kushawishi umma kujiunga na bima na kuwa na hifadhi kwenye mifuko ya kijamii.

Mkutano huo uliandaliwa na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sayansi Shirikishi Hochschule Bonn-Rhein-Sieg cha Ujerumani na kushirikisha wadau mbalimbali wa kifedha.

Alisema utafiti uliofanyika nchini mwaka jana na Finscope, ulibaini kuna elimu duni na imani duni kuhusu uwekezaji katika bima huku asilimia 11 waliohojiwa wakisema hawaoni manufaa ya mfumo wa bima, wakiwa na hoja ya mlolongo wa kunufaika na huduma hiyo ni mrefu.

"Wengi hawakati bima wakisema ni kama uchuro. Yaani kuwa na bima ni kujiandaa kupatwa na mambo mabaya.

"Mtu anaona kwanini niweke fedha, nisipoumwa je? Au anafikiri kwanini niweke fedha kwa ajili ya pensheni? Nisipofika uzeeni? Dhana ni nyingi na potofu," alisema Njovu.

Alitoa wito kwa watoa huduma za bima kuwa wabunifu na kufuata nyayo za mfumo wa taasisi za kifedha nchini, kumpatia mteja huduma ya fedha popote alipo kwa kutumia simu na kufanya miamala muda wowote pale wanapoishi.

Njovu alisema kuna pengo kuhusu uelewa wa umuhimu wa kuwa na bima na pensheni kutokana na huduma hizo kumlazimu mteja kuzifuata katika ofisi huku taasisi za kifedha zikiwa na mbinu rafiki zinazomshawishi mteja.

Mkuu wa Kitivo cha Bima na Benki wa IFM, Dk. John Kingu, alisema ili wananchi wavutiwe na bima kuna haja kuwapo sera rafiki na kuongezwa elimu kwa umma ili kuondoa dhana kwenye jamii kuwa bima ni uchuro.

Zubeda Chande, Mkuu wa Idara Hifadhi ya Jamii IFM, alisema kuna haja kufanya tena utafiti ili kuja na mpango wa elimu shirikishi na kujibu maswali ambayo yamo kwenye jamii.

# Mtaalamu Hisabati afukua mzizi wa kufeli kusikoisha

**Na Joyce Lameck**

DICKSON Haji (37), mtaalamu wa Hisabati aliyehitimu Shahada ya Sayansi ya Takwimu na Hisabati Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) ameorodhesha mambo yanayokwaza ufaulu katika somo hilo, ukiwamo ulevi wa michezo ya kubahatisha (kubeti).

Mkazi huyo wa Kata ya Mwaya, wilayani Kilombero, mkoani Morogoro, ameelekeza sehemu kubwa ya lawama kwa walimu wenzake, huku hisa inayobaki ni ya kitabia kwa wanafunzi wao.

Katika mazungumzo na mwandishi wa habari hizi jana katika ofisi za Nipashe, Mikocheni, Dar es Salaam, mtaalamu huyo alisema kuwa kwa miaka mitano anasimamia programu ya masomo ya ziada kwa masomo la Hisabati na Sayansi.

Alisema kuwa tangu ahitimu masomo yake mwaka 2012, amekuwa akifanya utafiti kubaini sababu za wanafunzi wengi kufeli somo la Hisabati nchini kwa kuanzisha kituo atamizi cha kupima kama jambo linalofikirika linaweza kuleta manufaa.

Kituo hicho alikipa jina la NMCCE INSCURATION CENTRE, akilenga kusaidia wanafunzi kwenye Sayansi na Hisabati, masomo ambayo ufaulu wake ni duni nchini.

Alisema ufuatiliaji wake kwa kipindi cha zaidi ya miaka 19, umebaini watoto wanakumbana na changamoto zinazosababisha ufaulu wao kuwa duni katika somo la Hisabati, tatizo hilo likitajwa kuwa janga la kitaifa.

Mtaalamu huyo alisema amebaini walimu wenzake kukosa umahiri wa ufundishaji somo hilo, akisisitiza kuwa mwanafunzi akisimamiwa vizuri na kufundishwa Hisabati, anaweza kuwa mbunifu, hata kwenye vitu tofauti.

Alisema aligundua kuna changamoto ya wanafunzi kufundishwa vitu visivyokuwa na uhalisia kutokana na vitabu vinavyotumiwa kufundishia somo hilo, pia serikali kutokufuatilia mambo yanayoendelea kwenye shule za umma.

"Mfano, tablets walizopewa kwa ajili ya matumizi ya masomo na kufanyia kazi za shule zimekuwa na matumizi tofauti kwa walimu kutumika kupekuruzi mitandaoni na si msaada kwa mambo ya kimasomo. Hiyo yote ni kwa sababu hawafuatiliwi na serikali," alisema.

Alisema kubeti pia ni changamoto mojawapo inayosababisha watoto kufeli katika mitihani yao kutokana na kutumia muda mwingi kuwaza kupata fedha kupitia michezo ya kubahatisha na kufuatilia kama wana uhakika wa kupata ushindi.

Baada ya kubaini changamoto hizo, mtaalamu huyo alisisitiza ndio sababu iliyompa msukumo kutoa mapendekezo kwa mamlaka ya elimu, ili kufanyiwa kazi na kuongeza ufaulu katika somo hilo.

Alipendekeza kila shule iwe na mtakwimu kuanzia ngazi ya shule ya msingi na sekondari, kwa kuwa mtakwimu ni mtafiti, ana uwezo wa kujua sababu za mtoto kufeli somo la mwalimu husika.

Mtaalamu Haji pia alisema lugha ya kufundishia shuleni kuanzia ngazi ya shule ya msingi inapaswa kuangaliwa, akipendekeza Kiswahili na Kiingereza vitumike kwa pamoja ili kusiwe na kikwazo cha lugha kwa mwanafunzi na awe uwezo wa kuelewa maswali katika lugha zote mbili.

Pia alipendekeza wajitokeze wadau watakaowezesha mashindano kwenye somo la Hisabati, kutahamasisha wanafunzi kushiriki na washindi kupewa zawadi, hivyo wengi kupenda somo hilo badala ya michezo ya kubashiri.

"Ni muhimu serikali ifanye maboresho ya mafunzo ya walimu kwa shule za msingi kwa sababu walimu wengi hawana umahiri katika baadhi ya mada ngumu za Hisabati kama vile maumbo, sehemu, vipimo, mafumbo na takwimu.

"Pia njia za ufundishaji shuleni ziboreshwe, hasa kwa wanafunzi wa darasa la tano, sita na saba; wapewe kazi za kufanya na kuwasilisha kwa kufanya matendo mbele ya darasa, wapewe mazoezi kwa makundi na hata mmoja mmoja na mwalimu aendeshe mjadala na wanafunzi ili kuwafanya wajiamini," alishauri.

## MIAKA 3 YA SAMIA

# Aenda na staili ya vitendo kuliko maneno mengi

**Na Christina Mwakangale**

UNAPOSIKIA kwenye vyombo vya habari kwa nchi yoyote, kiongozi wa taifa, kama vile rais ni mwanamke, kitu gani kinakujia kichwani? Ni mtazamo wa jinsi au jinsia?

Kwa nchi za kiafrika, Tanzania ikiwamo, kuwa kiongozi mwanamke, kuna mitazamo tofauti katika jamii ama hasi au chanya. Pamoja na dhana hizo, wako wanawake waliozishinda.

Rais Suluhu Hassan, ni mmoja wa marais saba (kwa mujibu wa tovuti ya africa.com) wanawake waliotia fora barani Afrika. Kati yao wako walioingia Ikulu, japo kwa mpito yaani miezi michache tu, huku sita wakishika madaraka kamili.

Alipotwaa tu madaraka, ujumbe wake ulikuwa: "Na hapa naomba niseme tu kidogo, kwa wale ambao wana mashaka. Mwanamke huyu ataweza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nataka niwaambie aliyesimama hapa ni Rais."

Viongozi hawa wanawake, wameweka historia barani Afrika na duniani kote, huku dunia ikiendelea kupambana na nafasi za wanawake viongozi ili kufikia 50/50. Nia hasa ni kuvunja mkwamo wa kijinsia na kuwa na uongozi shirikishi wenye usawa.

Machi, 2021 Rais Samia alitangazwa rasmi na kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kifo cha Rais John Magufuli. Akiwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo wa juu zaidi katika historia ya nchi ya miaka 63 ya uhuru hivi sasa.

Kimataifa, kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo, 2021 na 2022, ametajwa na taasisi za kimataifa likiwamo jarida la Forbes kuwa miongoni mwa viongozi wanawake 100 (Forbes: The World's 100 Most Powerful Women-2021) wenye ushawishi duniani.

Kadhalika mwaka 2022, taasisi ya kimataifa ya Avance Media, iliwatambua wanawake kutoka Afrika kupitia mradi wa kuwawezesha wasichana 'Be A Girl' ikiwatambulisha Wanawake 100 Waafrika Wenye Ushawishi Zaidi (100 Most Influential African Women), Samia akiwamo.

Mengi aliyoyafanya Rais Samia, yamo anayoyabeba kama kiongozi yeyote bila kujua jinsi, ingawa kwa tafsiri nyingine moja kwa moja, anabebwa na sura zote, akisimama kama kiongozi, mwanamke na mama.

Usemi kwamba 'Mcheza Kwao Hutuzwa'. Huu unalenga kuwapa moyo na hamasa waliofanya vizuri. Rais Samia, aliwarejeshea tabasamu mabinti waliokatiza masomo wakiwa shuleni kutokana na sababu tofauti lakini kubwa zaidi ni ujauzito.

Akiibeba ajenda ya dunia ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG 2030), aliwahamasisha wasichana kurejea masomoni baada ya kujifungua. Mabinti hao ni kati ya wale ambao walikuwa na ndoto ya kuwa kama mwanamke fulani na kuiongoza jamii kuanzia ngazi ya mtaa hadi taifa.

Rais Samia anafuata mkondo wa kauli za awali kutoka viongozi wa kimataifa. Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Irina Bokova, mwaka 2017 alisema elimu ya mtoto wa kike ni muhimu katika kusaidia kutimiza malengo ya SDG ifikapo mwaka 2030 ambalo ni lengo namba nne linalohusu elimu.

"Bila kuhusisha wasichana katika elimu, bila kushughulikia vikwazo muhimu katika elimu yao kama ubaguzi, vikwazo vya umaskini, ukabila na dini, hatuwezi kufikia uendelevu katika malengo yoyote ya elimu na malengo mengine ya maendeleo endelevu," anasema.

Rais Samia, katika baadhi ya mambo aliyoyatazama kwa ukaribu na kwa jicho la kijinsia, ni kufanikisha elimu ya juu kuwafikia wote, kwa kutenga Sh. bilioni 70 zaidi ya Sh. bilioni 500, kuhakikisha wanafunzi wote wanapata mkopo kwa ajili ya elimu ya juu mwaka 2021.

Pia alitangaza kuwaruhusu wanafunzi waliokatiza masomo kwa kwa sababu mbalimbali, ikiwamo ujauzito, kurejea masomoni huku akiongeza vyumba vya madarasa na kutenga Sh. bilioni 125 kwa ajili ya kukamilisha maboma 10,000 mwaka huo.

**AVUNJA DHANA**

Wakati akielekea kutimiza miaka mitatu Machi 19, mwaka huu, tangu aapishwe kuwa Rais, Nipashe inamwangazia kwa namna tofauti, ikiwamo mtazamo wa jinsi na jinsia, akivunja dhana hasi zilizotopea miongoni mwa wanajamii.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Rais Samia alieleza mambo mengi, bila kuacha kuirejea kauli aliyojitamkia awali hadharani na umma kumshangilia.

Katika mahojiano mwishoni mwa wiki iliyopita, Samia alitaja hatua alizopitia hadi kukifikia kiti cha urais, akianzia jimboni kuwa mwakilishi Makunduchi, Kisiwani Zanzibar na itaja namna ilivyokuwa changamoto jamii kumpokea.

"Wakati wa lile tamko, nilikuwa nimekumbuka kutiana moyo katika mambo ya maisha. Unajua wanaume wanapofanya jambo na akielekea kushindwa, anaambiwa 'mrume' hujikaza, nenda nenda, kwa hiyo na mimi sikuile, nikasema hapa 'mrume' hujikaza.



"Bila kujua au kuwa na uhakika naenda kufanya nini, nikasema nisimame. Niwahakikishie Watanzania kwamba aliyesimama hapa ni rais wa Tanzania, na nimesema vile nikijua changamoto iliko na wasiwasi ulioko mioyoni kwa watu.

"Ni mara ya kwanza kupatwa na hali ile tuliyokuwa nayo...wengi waliingiwa na hali ya 'shock' (mshtuko), lakini anayeingia angekuwa 'jibaba' mwenye misuli angalau kidogo wangetulia. Lakini anaingia mwanamke mwenye vishungi vyake, anasema kwa wepesi zaidi, na anatizama kama hataki.

"Nadhani wasiwasi mkubwa zaidi ulikuwa kwenye watu. Ile ilikuwa ndiyo changamoto yangu ya kwanza, nina msiba, lazima nivuke salama na aliyemama lazima aonyeshe kwamba nchi inaweza kuvuka. Ule ulikuwa mtihani wangu wa kwanza. Siyo siri mara ya kwanza niliposhika madaraka joto nililisikia," alisema.

Anaikumbushia kauli hiyo kila mara na walioko kwenye hadhira huinuka kumshangilia, kwa tafsiri nyepesi kwamba 'yaliyomo yamo', jinsi na uongozi, kwenye jamii za Kiafrika kuna neno.

"Na watu walilipuka kwa shangwe, kwamba kweli tumepata rais...kilichonisukuma kusema... ni tayari kulikuwa na minong'ono ataweza kweli huyu hebu angalieni, inawezekana.

"Rais haina 'gender' (jinsi), rais ni rais tu. Mamlaka ni mamlaka tu. Hofu isingeacha kuwapo kwa watu wote, kwanza kupoteza rais aliyekuwa madarakani, pili mwanamke anaingia pale, kure-place."

Anafafanua tangu dhamira yake iliyokuwapo awali moyoni mwake, akipenda kuwa mhudumu wa kwenye ndege (air hostess) na dhamira yake ikikatizwa na baba yake, aliyetamani bintiye airithi taaluma yake ya ualimu.

"Enzi zetu wakati huko shule, wala huwazi utakuwa nani nilikuwa naona ATCL (sasa ATCL)... ukiona 'airhostess' wanavyovaa, wanapendeza kweli, nikatamani kuwa kama wale, lakini masomo yangu yalikuwa sayansi.

"Lakini baba yangu mzazi alikuwa mwalimu. Nilipomaliza kidato cha nne, akanipangia kwenda ualimu lakini usiku uleule, nikatoroka baadaye nikawa karani. Nakumbuka nilikuwa mfano wa kupewa adhabu shuleni...ili iwe mfano kwa wengine," anasema.

**MARAIS BARANI**

Katika Afrika, wako marais tisa waliofikia hatua kama ya Rais Samia, wakishika mamlaka ya kuiongoza nchi kwenye nchi zao, wakiweka historia na rekodi, kwa jicho la dhana ya jinsi na jinsia.

Kwa nchi za Kiafrika, mgawanyo wa majukumu hutofautiana kulingana na jinsia kwamba mwanamke jukumu lake ni kama vile kupika, kuteka maji, wakati jinsi, ni tofauti za kibaolojia ambazo majukumu yake hayaingiliani, mfano mwanaume hawezi kubwa jukumu la ujauzito.

Marais hawa walitia fora wakiziongoza nchi zao, huku vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi, wakiwaangalia kila uchao, yale wanayoyamudu, kwa kuwa wengi wao nchini mwao ni mara ya kwanza kuwa na kiongozi mwanamke.

Ellen Johnson Sirleaf, akiwa Rais wa Liberia kuanzia Januari, 2006 hadi Januari 2018, ni mmoja wa wanawake hao. Mwingine ni Sahle-Work Zewde wa Ethiopia, bado yumo madarakani kuanzia Oktoba mwaka 2018 hadi sasa.

Yumo pia Ameenah Gurib-Fakim, aliyekuwa Rais wa Mauritius, kuanzia Juni mwaka 2015 hadi Machi mwaka 2018. Mwingine Catherine Samba-Panza, alikuwa Rais wa Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), Januari, 2014 hadi Machi, 2016.

Joyce Banda wa Malawi, naye aliweka rekodi akishika madaraka kwa nchi hiyo tangu Aprili mwaka 2012 hadi Mei mwaka 2014. Sylvie Kinigi, alishika madaraka akiwa Rais wa mpito wa nchi ya Burundi, kuanzia Oktoba, 1993 hadi Februari, 1994.

Agnès Monique Ohsan Bellepeau, alikuwa rais pia wa mpito wa Mauritius, tangu Machi, 2012 hadi Julai, 2012 na Mei mwaka 2015 hadi Juni 2015. Rose Francine Rogombé, alikuwa Rais wa mpito nchi ya Gabon, kuanzia Juni mwaka 2009 hadi Oktoba 2009.

# Aliyeua wanawe kwa soda yenye sumu naye afariki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU tano baada ya Dainess Mwashambo (30), kuwaua wanawe wawili kwa kuwanywesha sumu, naye amefariki dunia wakati akiendelea na matibabu.

Mwanamke huyo, mkazi wa Kijiji cha Mashesye, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, ambaye aliwaua wanawe Mario Adamson (4) na Beonis Adamson (2), huyo alikuwa amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya.

Anadaiwa kufanya tukio hilo Machi 5, mwaka huu, kwa kuwanywesha watoto hao soda iliyokuwa imechanganywa na sumu ya kukaushia majani aina ya Pare Force kisha na yeye kuinywa kwa lengo la kujiua, ili kuepuka aibu baada ya kutuhumiwa kwa wizi kijijini hapo.

Machi 6, Mwashambo pamoja na watoto wake walizidiwa na kupelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya kwa lengo la kuokoa maisha yao lakini walifariki dunia wakiendelea na matibabu.

Baada ya watoto hao kufariki dunia, mama yao aliendelea kutibiwa katika hospitali hiyo huku akiwa chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi na alikuwa anatarajiwa kuchukuliwa hatua za kisheria baada ya hali yake ya kiafya kuimarika.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Benjamin Kuzaga, alisema mama huyo alifariki dunia Jumamosi iliyopita jioni wakati akiendelea kupatiwa matibabu.

"Mtuhumiwa huyu alifariki Machi 9, saa 10:15 jioni alipokuwa anaendelea na matibabu akiwa chini ya ulinzi. Niwaombe wananchi wasijichukulie sheria mkononi kwa sababu kwanza ni kinyume cha sheria lakini inasababisha madhara kwa watu wasiokuwa na hatia kama ambavyo imetokea kwa watoto," alisema Kuzaga.

Aliwataka wananchi wanaokumbwa na matatizo, yakiwamo ya kifamilia, kutoa taarifa polisi hasa dawati la jinsia au kuwatumia viongozi wa serikali za vijiji.



Ofisa Biashara Mkuu Wilaya ya Kinondoni, Philipo Mwakibete, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam juzi wakati akitoa ufafanuzi wa matumizi ya kituo kipya cha daladala cha Mwenge. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Adaiwa kupewa ujauzito na kaka yake

**Na Shaban Njia,** KISHAPU

MWANAFUNZI wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Uchunga, Kishapu mkoani Shinyanga (jina limehifadhiwa) amekatisha masomo yake baada ya kudaiwa kupewa ujauzito na kaka yake wa kambo aliyefahamika kwa jina la Paul Kashindye.

Kaka yake huyo, mkazi wa Kijiji cha Unyenyembe Kata ya Uchunga mkoani humo, anadaiwa kutokomea kusikojulikana baada ya kufanya kitendo hicho.

Mpaka sasa mwanafunzi huyo ana ujauzito wa miezi saba na amehifadhiwa na kulelewa katika kituo cha malezi cha Agape Aids Control mpaka atakapojifungua baada ya kutishiwa na familia juu ya tukio hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema Jeshi la Polisi linamtafuta mtuhumiwa ili afikishwe katika vyombo vya sheria.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni tamaa za kimwili na kwamba Kashindye alikuwa akimbaka mdogo wake nyakati za usiku na muda wa kwenda kuchota maji kisimani hadi kumpa ujauzito na alipoona imejulikana, alitoroka nyumbani na kutokomea kusikojulikana.

Awali, mwanafunzi huyo akisimulia tukio hilo, alisema alikuwa akiingiliwa kwa nyakati tofauti na kaka yake hususani muda wa kutoka shule, nyakati za usiku akiwa amelala na wakati mwingine akienda mtoni. Alisema alipokuwa akitoa taarifa, ndugu zake hawakumjali wala kumsikiliza.

"Mama yetu alifariki dunia sisi tukiwa wadogo. Baba yetu alioa mke mwingine ambaye alikuwa na watoto wakubwa kina Paul ambaye sisi tumelelewa kwa mama wa kambo. Nilijaribu kueleza kuhusiana na tukio hili aliniambia nikisema halafu kaka akakamatwa na polisi atanichinja na baba yetu alishakimbia familia yuko Kahama," alisema.

Alisema baada ya ujauzito kukua, alifukuzwa shule akawa anaishi nyumbani ndipo walimu walipotoa taarifa kwa maofisa ustawi wa jamii ambao walimchukua na kumpeleka katika kituo cha Malezi cha Agape kutokana na kukosa msaada kwenye familia kutokana na manyanyaso kuzidi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Unyenyembe anakoishi mwanafunzi huyo, Shija Mwandu, alikiri kuwapo kwa tukio hilo lakini alisema ofisi yake haikushirikishwa kwa namna yoyote ili kumchukulia hatua mtuhumiwa na alipofuatilia alibaini binti alikuwa akitishwa na wanafamilia iwapo angetoa taarifa.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Wanawake Laki Moja, Anascholastica Ndagiwe, alisema matukio ya namna hiyo yamekuwa yakitokea kwenye familia na kusababisha wanafunzi kukatisha ndoto zao za masomo.

Mkurugenzi wa Kituo cha Malezi ya Watoto cha Agape Aids Control, John Myola, alikiri kumpokea mwanafunzi huyo na walipompeleka Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga, alibainika kuwa na ujauzito wa miezi saba.

Mbali na kubainika kuwa mjamzito, pia aligundulika kuwa na upungufu wa damu na lishe kutokana na kuishi katika mazingira magumu.

## Nyumba ya wakili yabomolewa kumpa haki mjane 'aliyepokwa'

**Na Remmy Moka,** SAUT

NYUMBA ya Wakili Joseph Mugabe, mkazi wa Ilemela mkoani Mwanza, anayedaiwa kujimilikisha ardhi ya mjane Rose Chacha kinyume cha sheria, imebomolewa kupisha haki ya mjane huyo aliyoitafuta kwa takribani miaka saba.

Nipashe ilishuhudia ubomoaji huo uliofanyika juzi kutokana na agizo la Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, alilolitoa wakati wa Kliniki ya Ardhi iliyoanza juzi mkoani hapa baada ya kusikiliza kilio cha mjane huyo.

Awali, akiwasilisha kero kuhusu kudhulumiwa kiwanja na wakili huyo, Rose alisema wakili huyo alikuwa mtetezi wa mmoja wa watu waliokuwa wakishtakiana na mume wake juu ya umiliki wa kiwanja. Alisema katika shauri hilo wadaiwa hao walishindwa, hivyo kuamuliwa kubomoa nyumba waliyokuwa wamejenga.

Alisema licha ya kushindwa shauri hilo na kuzuiwa kujenga katika eneo hilo, aliendelea na ujenzi wakati huo mjane akifuatilia kibali cha ujenzi, hivyo kutumia nafasi na fedha zake kuendelea kumyanyasa hadi kusababisha kuwekwa mahabusu alipotolewa na aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Kiomoni Kibamba.

"Ninatambua mchango wa mkurugenzi ambaye kwa sasa amehamishiwa Jiji la Mwanza. Alinisaidia kwa kiasi chake lakini bado mtu huyo anaendelea na manyanyaso kwa kuendelea kutumia kiwanja changu. Naomba serikali iingilie kati suala hili nipate haki yangu," aliomba Rose.

Akithibitisha kuwapo kwa mgogoro huo, Kibamba alisema mjane huyo ana haki halali ya umiliki wa kiwanja hicho kwa kuwa mamlaka husika zilithibitisha suala hilo na iliwahi kuamuru mara ya kwanza nyumba iliyojengwa ivunjwe.

Alisema Wakili Mugabe aliwahi kutakiwa kuachia kiwanja hicho lakini alikaidi na kujenga tena kwa mara ya pili bila kujali amri halali za serikali.

Baada ya kusikiliza hoja hizo na kufuatilia vithibitisho vya nyaraka za umiliki wa kiwanja hicho, Naibu Waziri Pinda aliagiza Idara ya Ardhi, Manispaa ya Ilemela kupeleka watu mara moja kubomoa nyumba hiyo na kumchukulia hatua za kisheria wakili huyo.

Aidha, alizitaka idara za ardhi mkoani hapa kuhakikisha zinatenda haki kwa kufuata kanuni na taratibu husika wanapowasikiliza wenye kero kama hizo na si kuangalia uwezo wa mtu katika kutoa haki.

Pinda aliwataka wananchi kuchukua hatua stahiki za kisheria pale wanapokutana na migogoro ya ardhi kuliko kukaa nayo bila kupatiwa ufumbuzi hali inayosababisha kudhulumiwa moja kwa moja.

# Waandishi waachia nyumba ya Mbowe

Na Mwandishi Wetu

WAANDISHI wa habari 10 wanaomdai Mkurugenzi wa Tanzania Daima, Dudley Mbowe, Sh. milioni 62.7 wameachia nyumba ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, waliyoikamata ili ipigwe mnada.

Hata hivyo, waandishi hao wamegoma kulipa gharama za kesi kwa sababu hata wao wanaingia gharama katika kudai haki yao.

Hayo yalibainika jana Mahakama Kuu ya Tanzania Divisheni ya Kazi mbele ya Naibu Msajili, Mary Mrio, wakati shauri hilo likisikilizwa.

Mbowe kupitia wakili wake, John Mallya, aliwasilisha maombi chini ya kiapo kilichoapwa na Mbowe, Februari 26, mwaka huu, akitaka wajibu maombi kuondoa nyumba hiyo kwa sababu si mali ya Dudley na mahakama iwaamuru wajibu maombi hao kumlipa gharama za kesi mteja wake.

Kulwa Mzee, kwa niaba ya wajibu maombi, alidai walipitia nyaraka zote na viambatanisho na wamejiridhisha na kukubaliana kwa pamoja kwamba nyumba waliyoikamata ni ya familia, lakini inamilikiwa na Mbowe.

“Mheshimiwa tumepitia nyaraka pamoja na viambatanisho ikiwamo hati ya nyumba. Tumejiridhisha kwamba mkurugenzi tunayemdai, Dudley Mbowe, si mmiliki, hivyo tunaiomba mahakama tuiondoe nyumba hiyo kwenye maombi yetu.

“Kuhusu gharama Mheshimiwa, kwa uelewa wetu kwa mashauri ya migogoro ya kazi, hakuna gharama na hiyo inatokana na uwezo wa vipato vidogo vya wafanyakazi.

“Wakati sisi tunafanya hili jambo tulikuwa tukiamini kabisa kuwa ni nyumba ya mkurugenzi wetu kwa sababu katika hatua ya makubaliano, alikuwa anatuambia kuwa tutafanya vikao nyumbani kwake na tumefanya hapo vikao kwenye hiyo nyumba.

“Mheshimiwa katika hatua za mwisho, baba yake ambaye ndiye mwombaji katika shauri hili, alitualika tukutane hapo hapo ambapo tulikuwa tunakutana na tulikutana hapo, akakubali kubeba dhamana ya mtoto wake akakubali kutulipa mwezi Desemba,” alidai Kulwa.

Kulwa alidai kutokana na mazingira hayo waliamini kuwa hapo ndipo nyumbani kwake mkurugenzi na baada ya kushindwa kuwalipa katika kutekeleza namna ya kupata haki yao ndio maana waliamua kukamata hiyo nyumba.

“Kwa hiyo Mheshimiwa, tunaomba tusilipe gharama. Kwanza, huyu mwombaji hajaingia gharama kwani katika hatua zote za majadiliano tulikuwa tunakwenda kwake kwa gharama zetu wenyewe na ahadi zake za kutulipa Desemba baada ya kushindwa kutekeleza hilo, liliituathiri maana tulikuwa katika maandalizi ya sikukuu na ada za watoto shuleni,” alidai Kulwa.

Kulwa aliomba Mahakama katika uamuzi kuhusu gharama ikiwezekana kila upande ubebe gharama zake.

Dalali wa Mahakama, Jesca Massawe, alidai alipokea amri ya mahakama kwa ajili ya kukamata nyumba hiyo.

“Sisi kama madalali wa mahakama katika kutekeleza majukumu yetu, tulikaa na mahakama hii chini ya Jaji Mfawidhi akatuelekeza kuwa katika mashauri haya ya kukamata mali, tusijihusishe na utambuzi wa mali bali tukamate na kama kuna changamoto basi italetwa mahakamani,” alidai na kuongeza kwamba alitekeleza amri ya mahakama kama ilivyoelekezwa.

Akijibu hoja hizo, Wakili Mallya alidai anakubaliana na mjibu maombi Kulwa kwa aliyoyasema ya kuachia nyumba hiyo.

“Kuhusu suala la gharama mteja mwombaji anastahili kulipwa gharama na mambo mengine aliyoyasema mjibu maombi alipaswa kuyaleta kwa njia ya kiapo,” alidai Mallya.

Kuhusu hoja za mjibu maombi wa 11 ambaye ni dalali, alidai kuwa kweli ni ofisa wa mahakama, lakini maelezo yake hayakuja kwenye kiapo.

“Kwa kuwa anamtaja Jaji Mfawidhi, haya yalipaswa kuja kwa njia ya kiapo na si maneno matupu mahakamani. Kwa hiyo naiomba mahakama yako isiyazingatie na tunaomba mahakama izingatie suala la gharama,” alidai Mallya.

Naibu Msajili Mrio, baada ya kusikiliza hoja za pande zote, aliahirisha shauri hadi leo saa 8:00 mchana kwa ajili ya uamuzi.

Katika shauri la msingi, mjibu maombi mwingine Maregesi Paul aliomba kuyaondoa maombi ya kukamata nyumba hiyo na kuieleza Mahakama kwamba wanatarajia kuwasilisha maombi mengine upya ya kumkamata Dudley.

“Maombi haya yameondolewa kwa kibali cha kuyaleta tena,” alisema Msajili.

Mbowe amefungua shauri dhidi ya Maregesi Paul, Fidelis Felix, Christina Mwakangale, Janeth Josiah, Exuperius Kachenje, Hellen Sisya, Kulwa Mzee, Nora Damian, Makuburi Ally, Mkurugenzi wa Gazeti la Tanzania na Kampuni ya Udalali ya JJ Auctioneers & Debt Collectors.

Februari 13, mwaka huu, mahakama ilikubali maombi ya wadai na kumteua dalali wa mahakama kukamata nyumba kwa ajili ya kuipiga mnada.

Februari 28, mwaka huu, dalali Jesca Massawe alibandika matangazo ya kukamata nyumba ya mkurugenzi tayari kupigwa mnada kufidia deni la malimbikizo ya mishahara wafanyakazi.

Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Mary Mrio, alitoa amri hiyo baada ya kupitia hoja za washinda tuzo katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Julai, 2023. Shauri hilo namba 28461 la mwaka 2023, wadai ni Maregesi Paul na wenzake tisa dhidi ya Mkurugenzi wa Gazeti la Tanzania Daima, Dudley Mbowe.

Baada ya mdaiwa kukaidi kulipa, wadai walikubaliana njia sahihi ni kukamata nyumba yake Na. 9 iliyopo Mtaa wa Feza, Mikocheni B barabara ya Chipaka na Mahakama ilikubali.

Walalamikaji hao walipata tuzo Julai 17, 2023 mbele ya Msuluhishi wa CMA Ilala, Bonasia Mollel.

Madai ya awali yalikuwa jumla Sh. milioni 114 baada ya kukaa mezani kwenye majadiliano kwa pamoja kiwango hicho cha fedha, kilishuka hadi kufikia Sh. milioni 62.7.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA HUDUMA YA TATHMINI HURU YA UTEKELEZAJI WA MPANGO KAZI WA UHAMISHAJI WA WATU NA MAKAZI KWA AJILI YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (TANZANIA): KUMBUKUMBU NA: REQ-00000492**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP LTD), inakaribisha makampuni au Mashirika zenye uwezo na uzoefu wa kutathmini utekekelezaji wa Mipango ya Uhamishaji wa Watu na Makazi ya Mradi wa Bomba la Mafuta la Ghafi la Afrika ya Mashariki (EACOP) kwa upande wa Tanzania.

Mradi wa EACOP unahusisha a ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirishwa kwenye masoko ya kimataifa.

Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Rasi ya Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443 kati yake kilomita 296 zitakuwa nchi ya Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. . Kwa Tanzania, Bomba la mafuta litapita katika Mikoa nane (8) inayojumuisha Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA**

Mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (hapa ikijulikana kama “Mradi”) umetwaa ardhi zaidi ya ekari 8,800 kwa ajili ya ujenzi wa Bomba pamoja na miundombinu ya juu, ambapo takribani waguswa 10,000 wamepitiwa na mradi huu kwa upande wa Tanzania. Jumla ya Mipango Kazi Kumi pamoja na Mpango Kazi Mmoja wa Nyongeza wa Utekelezaji wa Uhamishaji wa Watu na Makazi imeandaliwa na kuonyeshwa kwa Umma. Katika kila Mpango Kazi kuna Mpango Mahsusi kwa ajili ya Urejeshaji wa Hali za Maisha za Waguswa. Ardhi kwa ajili ya shughuli za Mradi wa Bomba la Mafuta imetwaliwa moja kwa moja, Hati za Umiliki wa Ardhi hiyo kukabidhiwa kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na ardhi hiyo kukodishwa kwa Kampuni ya EACOP. Zoezi la kuonyesha stahiki za waguswa, kusaini mikataba ya fidia na kulipa fidia zimekamilika kwa asilimia tisini na tisa (99%). Ujenzi wa Nyumba mbadala za waguswa umekamilika na nyumba zote kukabidhiwa kwa waguswa. Muda wa ukomo wa tangazo la watu kuondoka kwenye maeneo ya mradi ulikamilika mwezi Julai 2023 na shughuli za Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi zinaendelea.

Kulingana na Vipengele vya Ufuatiliaji vilivyoainishwa kwenye Mipango Kazi hiyo, Mradi unapaswa kufanya Tathmini mbalimbali za Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi pamoja na kukamilisha Ukaguzi wa miaka mitatu baada ya waguswa kuondoka kwenye maeneo ya Mradi. Tathmini hizi zitatoa taswira ya kama Malengo ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Watu na Makazi yamefikiwa na kubainisha maeneo yenye mapungufu na yanayohitaji marekebisho.

Mradi unahitaji Kampuni au taasisi zenye sifa na uzoefu katika kufanya shughuli za Ukaguzi na Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi kwa mujibu wa Viwango vya Utendaji vya Mashirika ya Kimataifa ya Fedha, Matakwa ya Nne ya Ikweta, pamoja na Viwango vya Ubora wa Sekta ya Mafuta na Gesi Kimataifa.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni au Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa Usajili wa Kampuni kutoka katika Mamlaka zinazohusika na Usajili wa shughuli za Makampuni (BRELA) (Ambatanisha nakala yake)
- Leseni ya Biashara
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Kanzidata ya watoa huduma wa ndani ya nchi (LSSP) ya EWURA au uthibitisho wa maombi ya kusajiliwa kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia (Hili linasisitizwa sana)
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Maelezo na Uthibitisho wa uzoefu kwenye eneo la Utekekezaji na Ufuatiliaji wa Uhamishaji wa Watu na Makazi pamoja na Urejeshaji wa Hali za Maisha kwenye Miradi Mikubwa yenye umbali mrefu ndani ya Afrika.
- Nakala za Wasifu za wataalamu wabobezi katika utekelezaji na Ukaguzi wa Mpango wa Uhamishaji wa Watu na Makazi, pamoja na Urejeshaji wa Hali za Maisha za Waguswa.
- Uthibitisho wa Uzoefu katika kufanya tathmini, ukaguzi na uhakiki wa kina wa Utekelezaji wa Uhamishaji wa Watu na Makazi pamoja na Urejeshaji wa Hali za Maisha katika sekta binafsi au mashirika makubwa ya ukopeshaji fedha.
- Uthibitisho wa uwezo wa kifedha katika kutekeleza huduma hii ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa za Ukaguzi wa hesabu za fedha wa miaka mitatu iliyopita
- Uthibitisho wa mfumo wa Usimamizi wa Ubora, Afya, Usalama na Mazingira (QHSE) na mchakato wa kufuata viwango vya Serikali na Viwanda vinavyotumika kwa kazi inayofanana.
- Uthibitisho wa Sera za Kampuni za kupambana na rushwa, kupambana na kutoa hongo, kuzingatia wa Sheria na Usimamizi wa Haki za Binadamu.

Makampuni au mashirika yenye nia, na ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usiozidi Mb20) hadi kufikia saa **11:00 jioni** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **27/03/2024**. Kichwa cha Barua Pepe kiwe **REQ-00000492 TATHMINI HURU YA UTEKELEZAJI WA MPANGO KAZI WA UHAMISHAJI WA WATU NA MAKAZI - EACOP TANZANIA.**
**Maombi yote yakuonesh ania yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.**
**Maombi yote yawasilishwe kwa Lugha ya Kiswahili.**

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itakagua na kutathimini nyaraka zilizotumwa na makampuni au mashirika yaliyoonesha nia kulingana na Tangazo hili la nia ya kutoa huduma, na kisha kufanya tathmini kulingana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni au mashirika yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni au mashirika yenye vigezo. Mwaliko kwa makampuni au mashirika kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni au mashirika hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukata kampuni au shirika na kubaki na maamuzi yake bila kutoa sababu kwa makampuni au mashirika husika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Malori yatamaliza watu ajali za barabarani

**MATUKIO** ya ajali za barabarani ambayo husababisha vifo vya raia wengi yanaendelea kutokea siku hadi siku kutokana na uzembe wa baadhi ya madereva.

Ajali nyingi zinazoripotiwa baadhi yake zinasababishwa na uzembe wa madereva kwa kutozingatia sheria za usalama barabarani.

Mara kwa mara ajali za barabarani chanzo ni malori ambayo wakati mwingine yanaegeshwa barabarani bila kutoa tahadhari kwa magari mengine.

Madereva wa malori wanaweza kupita magari mengine bila kuangalia sehemu hiyo ni salama kufanya hivyo, lakini kutokana na ukubwa wa magari yao wanajua madereva wengine wa magari madogo wataogopa na kuwapisha.

Kuna baadhi ya ajali zinatokea kwa magari hayo kutokaguliwa kama yako salama kwa safari na matokeo yake yanapofika kwenye mteremko mkali na kunapotokea jambo la dharura, dereva anashindwa kulihimili na kuparamia magari mengine.

Watu wengi wanapoteza maisha kutokana na uzembe wa madereva wa malori kutaka kujiona wao ndio madereva bora barabarani.

Nyakati za usiku ndio huwa balaa zaidi kwa sababu unaweza kukuta lori limeegeshwa barabarani bila tahadhari. Kwa mfano hakuna kiashiria cha mwanga kinachoonesha kuna gari mbele hali inayosababisha madereva wengine ambao nao kwa kutokuwa na umakini huyaparamia.

Tukio kama hilo liliwahi kutokea Barabara ya Bagamoyo na kuua familia baada ya lori kuharibika barabarani na kutowekwa alama yoyote ya tahadhari na dereva aliyekuwa akiendesha familia hiyo kuliparamia kwa sababu halikuwekwa alama ya tahadhari.

Wapo pia madereva wanaojiona wana haraka ya kufika wanakokwenda na kuamua kuyapita magari mengine kwa mwendo kasi kiasi cha kusababisha inapotokea hatari kushindwa kusimama na kuparamia magari mengine.

Ni juzi tu katika barabara hiyo hiyo ya Bagamoyo kuna ajali ambayo imesababisha uhai wa watu tisa kupotea kwa sababu ya uzembe wa madereva.

Ajali hiyo ilitokana na lori lililokuwa limebeba mawe kutaka kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari na kwenda kukutana uso kwa uso na gari la abiria na kusababia vifo vya watu tisa na majeruhi saba.

Ajali zinazosababishwa na malori zinapoteza uhai wa watu na vilevile kuharibu miundombinu ya barabara.

Katika siku za hivi karibuni, katika barabara hiyo hiyo ya Bagamoyo eneo la Tegeta kwa ndevu, lori liliacha njia na kuparamia vizuizi vya daraja na kutumbukia kwenye daraja. Ajali hiyo iliua watu wote waliokuwa kwenye lori hilo.

Vifo vinavyotokana na hizo vinasikitisha kwasababu vinatokea kwa uzembe wa mtu mmoja. Wakati mwingine watembea kwa miguu wanakutana na ajali hizo baada ya madereva hao kuwafuata kwenye njia zao.

Wafanyabiashara wanaouza bidhaa zao kando ya barabara pia wapo hatarini kukumbwa na ajali hiyo kutokana na uzembe wa madereva.

Nyumba za watu pia zimepata misukosuko ya kuparamiwa na malori, wakati mwingine watu wakiwa wamelala na kukutwa na vifo.

Kuna umuhimu pia wa askari wa kikosi cha usalama barabarani kuyakagua malori hayo kuhakikisha yana usalama yanapokuwa safarini ili kuepusha ajali zinazotokea mara kwa mara.

Madereva wa magari hayo pia wanatakiwa kuwa makini wanapokuwa barabarani kwa kuwa ajali inapotokea maisha yao pia yanakuwa hatarini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Wanafunzi wote wanahitaji kula

**MIKOA** ya Njombe, Kilimanjaro, Arusha, Pwani, Iringa na Manyara, imesifika kwa kutoa chakula shuleni, kuchochea ubora na ufaulu kwa wanafunzi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, (anayeshughulikia elimu) Dk.Franklin Rwezimula, ndiye anayeitaja mikoa hiyo jijini Dodoma hivi karibuni kwenye maadhimisho ya Siku ya Afrika ya Chakula Shuleni.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri huyo, huduma ya chakula shuleni katika mikoa hiyo inapatikana kwa zaidi ya asilimia 80, na kwamba hatua hiyo inapunguza utoro kwa wanafunzi.

Mbinu zilizotumiwa na mikoa hiyo hadi huduma ya chakula shuleni kupatikana kwa zaidi ya asilimia 80 ni ya kuigwa na mikoa mingine, ili hatimaye wanafunzi wa shule zote wapate mlo.

Inaelezwa kuwa chakula shuleni kinachochea ubora na ufaulu kwa wanafunzi, hivyo ni vyema mikoa mingine ambayo bado yako nyuma ikaangaalia uwezekano wa kuwepo kwa chakula.

Kukosekana kwa chakula shuleni kunachangia utoro wa rejareja kwa wanafunzi na wengine kukatisha masomo, hivyo, serikali imeanzisha utaratibu wa kuishirikisha jamii kuchangia upatikanaji wa chakula

Tanzania bara ina mikoa zaidi ya 20, kwa nini ni mikoa sita tu ambayo chakula shuleni kipatikana kwa zaidi ya asilimia 80? Mikoa mingine ina changamoto gani hadi ishindwe kutoa huduma hiyo?

Si vibaya mikoa ambayo bado iko nyuma, ikaanza kazi ya kuhamasisha jamii, wadau wa elimu wakiwamo wazazi ili kuweka mikakati ya kutekeleza afua za lishe shuleni, kwa kuzingatia ushauri wa wataalam wa afya, wa saikolojia kuwa yapo madhara makubwa ya kukosekana kwa chakula kuwa ni njaa, usikivu, utoro wa rejareja na kukatisha masomo.

**Serikali inafanya sehemu yake katika huduma hiyo, wazazi na walezi nao wana sehemu yao katika kuhuduma shule hasa kwa kuzingatia kwamba shule hizo ni za umma, halafu wenyewe ndio umma.**

Ninaamini kuwa serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya elimu, lakini pia upatikanaji wa matokeo mazuri ya elimu hutegemea afya bora kwa wanafunzi, hivyo chakula shuleni ni muhimu.

Ingekuwa ni vyema kwa kila mdau wa elimu kutambua ushauri wa wataalam wa afya kuwa chakula shuleni ni muhimu, kwa kuwa kinachochea ubora wa elimu na ufaulu kwa wanafunzi.

Kwa kuwa jitihada za kuwasaidia wanafunzi kusoma vizuri na kupata matokeo mazuri ni kuwapo kwa chakula shuleni, basi jambo hilo lipewe uzito mkubwa ili kusiwe na shule ambayo haina huduma hiyo.

Ikumbukwe kuwa mwaka 2021.Wizara ya Elimu ilizindua Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma ya Chakula na Lishe kwa Wanafunzi wa Elimu msingi ili kuweka utaratibu wa kitaifa ambao utawezesha wanafunzi kula chakula.

Kimsingui, upatikanaji wa chakula shuleni ni suala mtambuka ambalo linahitaji ushiriki wadau wote wa elimu hasa wazazi na walezi, lakini mtindo wa baadhi yao kujiweka kando, unasababisha baadhi ya wanafunzi kukosa huduma hiyo muhimu kwa wanafunzi.

Wazazi na walezi wasiwe wazito kuchangia chakula na kusababisha watoto wao kushinda njaa, wakisingizia kuwa serikali ilishatangaza elimu bure, msimamo ambao ni wazi unawaathiri watoto wao kimasomo.

Serikali inafanya sehemu yake katika huduma hiyo, wazazi na walezi nao wana sehemu yao katika kuhuduma shule hasa kwa kuzingatia kwamba shule hizo ni za umma, halafu wenyewe ndio umma.

Ninadhani si sahihi mzazi au mlezi kugoma kupeleka shuleni kilo moja ya maharage na unga kwa ajili ya mtoto wake kwa kisingizio kuwa serikali inatoa elimu bure. Kama ndivyo, mchango wa watu wa aina hii katika shule zao ni upi? Ni vyema kila mmoja afanye sehemu yake.

# Wananchi kusambaziwa majiko yanayotumia umeme mdogo

**Na Beatrice Shayo**

ILI kusaidia wanawake kupata nishati safi ya jikoni, serikali na wadau wanakusudia kuwafikishia wananchi huduma hiyo kwa kushirikiana na wafanyabiashara.

Wafanyabiashara watasambaza majiko yanayotumia umeme kidogo wa uniti moja kupika chakula cha mlo mmoja kwa familia.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Nishati mbadala Tanzania (TAREA), Prosper Magali, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kampeni ya pika kijanja iliyoandaliwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kupitia stesheni ya Bongo FM.

Alisema nishati ambayo wanaihamasisha kwa wananchi ni kupika kwa kutumia umeme kwa sababu imeenea katika maeneo mengi nchini.

Alisema malengo ya serikali ni kusambaza umeme vijiji vyote na taasisi yake imebaini kupika kwa kutumia umeme ni nafuu zaidi kuliko vyanzo vingine.

"Unafuu huo unapatikana kama utatumia majiko haya ambayo tunayahamasisha haya majiko ya umeme ya presha ambayo yanatumia kiwango kidogo, lakini yametengenezwa kuhifadhi joto umeme unahitajika kwa ajili ya kuchemsha chakula lile joto linatumika kuivisha chakula," alisema Magali.

Alisema utafiti wao umeonyesha uniti moja ya umeme ambayo kwa sasa ni Sh. 400 inatosha kuivisha chakula cha mlo mmoja.

"Uniti tatu inatosha kwa matumizi ya kupika vyakula kwa siku nzima ukitazama gharama hizo na vyanzo vingine utaona kuna unafuu watu wanatumia zaidi ya Sh. 3,000 kwa siku kwa nishati ya kupika," alisema.

Mhandisi wa nishati kutoka Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Sayuni Mbwilo, alisema inaweza kuonekana matumizi ya nishati safi ni gharama jambo ambalo sio sahihi inategemea na aina ya vifaa ambavyo mtu anavitumia.

Mbwilo alisema katika mradi huo wamekuja na sera kwa Shirika la Viwango (TBS) litaenda kutengeneza viwango ambavyo majiko ya umeme yanayoingia nchini hayataingia ovyo tena.

Alisema kupitia mradi huo kuna maabara mbili ambazo zinamsaidia mwanamke anayepika aweze kujua jiko lake lina matumizi gani ili asiwe na gharama kubwa.

"Tunategemea lile wazo la Rais Samia Suluhu Hassan, la nishati safi kwa bei nafuu tunaenda kulifikia kwa sababu mradi umeangalia huo mlengo, lakini tutakuwa na kampeni kila mwananchi afahamu matumizi ya jiko ambalo halitakufanya kutumia nishati nyingi," alisema.

Mkurugenzi wa huduma za redio kutoka Shirika la Utangazaji la TBC, Aisha Dachi, alisema wanaunga mkono jitihada za wananchi kutumia nishati safi na kuachana na nishati chafu inayosababisha madhara kwa wananchi.

Alisema wamezindua kampeni hiyo itakayokuwa inatangazwa kupitia Bongo FM ya pika kijanja ambayo itakuwa endelevu kuhakikisha wananchi wanatumia nishati safi na salama.

Dachi alisema baada ya uzinduzi huo wataendelea kupitia vijijini na kufanya matamasha na kuwatafuta wadau wa nishati safi kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika katika maendeleo ya mitaji (UNCDF), Elizabeth Ngoye, alisema kuhama kutoka kwenye mkaa na kuni ni suala la taratibu kuna haja ya kuboresha sera ili kuwapo na utengenezaji bora wa mikaa na matumizi sahihi ya kuni.

Alisema wana mradi wa kutoa elimu kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupika chakula ili kupunguza madhara.



Balozi wa Kenya nchini Tanzania, Isaac Njenga (kushoto), akisalimiana na Mkuu wa Fedha wa KCB Bank Tanzania, Willis Mbatia, wakati wa mkutano wa raia wa Kenya waishio Tanzania, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Meneja wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kati wa Shirika la Ndege la Kenya (Kenya Airways), Dk. Joseph Munyeti. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mbowe, waandishi wanaomdai ngoma nzito

**Na Mwandishi Wetu**

WAANDISHI wa habari 10 wanaomdai Mkurugenzi wa Tanzania Daima, Dudley Mbowe, Sh. milioni 62.7 wameachia nyumba ya Freeman Mbowe waliyoikamata kuipiga mnada na kugoma kulipa gharama za kesi kutokana na kuingia gharama ya kudai haki yao.

Hayo yalibainika jana Mahakama Kuu ya Tanzania Divisheni ya Kazi, mbele ya Naibu Msajili Mary Mrio wakati shauri hilo likisikilizwa.

Mbowe kupitia Wakili John Mallya, aliwasilisha maombi chini ya kiapo kilichoapwa na Freeman Mbowe, Februari 26, mwaka huu akitaka wajibu maombi kuondoa nyumba hiyo kwa sababu sio mali ya Dudley na Mahakama iwaamuru wajibu maombi hao kumlipa gharama za kesi mteja wake.

Kulwa Mzee kwa niaba ya wajibu maombi alidai walipitia nyaraka zote na viambatanisho wamejiridhisha na wamekubaliana kwa pamoja kwamba nyumba waliyoikamata ni ya familia, lakini inamilikiwa na Freeman Mbowe.

"Mheshimiwa tumepitia nyaraka pamoja na viambatanisho ikiwamo hati ya nyumba, tumejiridhisha kwamba mkurugenzi tunayemdai Dudley Mbowe sio mmiliki hivyo tunaiomba mahakama tuiondoe hiyo nyumba kwenye maombi yetu.

"Kuhusu gharama mheshimiwa, kwa uelewa wetu kwa mashauri ya migogoro ya kikazi hakuna gharama na hiyo inatokana na uwezo wa vipato vidogo vya wafanyakazi.

"Wakati sisi tunafanya hili jambo tulikuwa tukiamini kabisa kuwa ni nyumba ya mkurugenzi wetu kwa sababu katika hatua ya makubaliano alikuwa anatuambia kuwa tutafanya vikao nyumbani kwake na tumefanya hapo vikao kwenye hiyo nyumba.

"Mheshimiwa katika hatua za mwisho baba yake ambaye ndiye mwombaji katika shauri hili alitualika tukutane hapo hapo ambapo tulikuwa tunakutana na akakubali kubeba dhamana ya mtoto wake kutulipa mwezi Desemba," alidai Kulwa.

Kulwa alidai kutokana na mazingira hayo waliamini kuwa hapo ndipo nyumbani kwake mkurugenzi na baada ya kushindwa kuwalipa katika kutekeleza namna ya kupata haki yao ndio maana waliamua kukamata nyumba hiyo.

"Kwa hiyo mheshimiwa tunaomba tusilipe gharama, kwanza huyu mwombaji hajaingia gharama kwani katika hatua zote za majadiliano tulikuwa tunakwenda kwake kwa gharama zetu wenyewe na ahadi zake za kutulipa Desemba baada ya kushindwa kutekeleza hilo lilituathiri maana tulikuwa katika maandalizi ya sikukuu na ada za watoto shuleni," alidai Kulwa.

Kulwa aliomba mahakama katika uamuzi kuhusu gharama ikiwezekana kila upande ubebe gharama zake.

Akijibu dalali wa mahakama, Jesca Massawe alidai alipokea amri ya mahakama kwa ajili ya kukamata nyumba hiyo.

Akijibu, Wakili Mallya alidai anakubaliana na mjibu maombi Kulwa kwa aliyoyasema ya kuachia nyumba hiyo.

"Kuhusu suala la gharama mteja mwombaji anastahili kulipwa gharama na mambo mengine aliyoyasema mjibu maombi alipaswa kuyaleta kwa njia ya kiapo," alidai Mallya.

Kuhusu hoja za mjibu maombi wa 11 ambaye ni dalali, alijibu kuwa kweli ni ofisa wa Mahakama, lakini maelezo yake hayakuja kwenye kiapo.

Naibu Msajili Mrio baada ya kusikiliza hoja za pande zote aliahirisha shauri hadi leo saa nane mchana kwa ajili ya uamuzi.

Katika shauri la msingi, mjibu maombi mwingine Maregesi Paul, aliomba kuyaondoa maombi ya kukamata nyumba hiyo na kuieleza mahakama kwamba wanatarajia kuwasilisha maombi mengine upya ya kumkamata Dudley.

"Maombi haya yameondolewa kwa kibali cha kuyaleta tena," alisema Msajili.

Mbowe amefungua shauri dhidi ya Maregesi Paul, Fidelis Felix, Christina Mwakangale, Janeth Josiah, Exuperius Kachenje, Hellen Sisya, Kulwa Mzee, Nora Damian, Makuburi Ally, Mkurugenzi wa Gazeti la Tanzania na Kampuni ya Udalali ya JJ Auctioneers& Debt Collectors.

Februari 13, mwaka huu, mahakama ilikubali maombi ya wadai na kumteua dalali kukamata nyumba kwa ajili ya kuipiga mnada.

Februari 28, mwaka huu, dalali wa mahakama, Jesca Massawe, alibandika matangazo ya kukamata nyumba ya Mkurugenzi kupigwa mnada kufidia deni la malimbikizo ya mishahara wafanyakazi.

Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Mary Mrio alitoa amri hiyo baada ya kupitia hoja za washinda tuzo katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), Julai 2023.

Baada ya mdaiwa kukaidi kulipa, wadai walikubaliana njia sahihi ni kukamata nyumba yake namba 9 iliyopo Mtaa wa Feza, Mikocheni B, barabara ya Chipaka na mahakama ilikubali.


Walalamikaji hao walipata tuzo Julai 17 mwaka 2023 mbele ya Msuluhidhi wa CMA Ilala, Bonasia Mollel.

Madai ya awali yalikuwa jumla ya Sh. milioni 114 baada ya kukaa mezani kwenye majadiliano kwa pamoja kiwango hicho cha fedha kilishuka na kufikia Sh. milioni 62.7.

Dudley alikubali kulipa fedha hizo kwa awamu tatu, Oktoba 30, Desemba 30 mwaka 2023 na awamu ya mwisho ilikuwa mwishoni Februari, mwaka huu, lakini hakulipa.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



## Wananchi kusambaziwa majiko yanayotumia umeme mdogo

**Na Beatrice Shayo**

ILI kusaidia wanawake kupata nishati safi ya jikoni, serikali na wadau wanakusudia kuwafikishia wananchi huduma hiyo kwa kushirikiana na wafanyabiashara.

Wafanyabiashara watasambaza majiko yanayotumia umeme kidogo wa uniti moja kupika chakula cha mlo mmoja kwa familia.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Nishati mbadala Tanzania (TAREA), Prosper Magali, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kampeni ya pika kijanja iliyoandaliwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kupitia stesheni ya Bongo FM.

Alisema nishati ambayo wanaihamasisha kwa wananchi ni kupika kwa kutumia umeme kwa sababu imeenea katika maeneo mengi nchini.

Alisema malengo ya serikali ni kusambaza umeme vijiji vyote na taasisi yake imebaini kupika kwa kutumia umeme ni nafuu zaidi kuliko vyanzo vingine.

"Unafuu huo unapatikana kama utatumia majiko haya ambayo tunayahamasisha haya majiko ya umeme ya presha ambayo yanatumia kiwango kidogo, lakini yametengenezwa kuhifadhi joto umeme unahitajika kwa ajili ya kuchemsha chakula lile joto linatumika kuivisha chakula," alisema Magali.

Alisema utafiti wao umeonyesha uniti moja ya umeme ambayo kwa sasa ni Sh. 400 inatosha kuivisha chakula cha mlo mmoja.

"Uniti tatu inatosha kwa matumizi ya kupika vyakula kwa siku nzima ukitazama gharama hizo na vyanzo vingine utaona kuna unafuu watu wanatumia zaidi ya Sh. 3,000 kwa siku kwa nishati ya kupika," alisema.

Mhandisi wa nishati kutoka Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Sayuni Mbwilo, alisema inaweza kuonekana matumizi ya nishati safi ni gharama jambo ambalo sio sahihi inategemea na aina ya vifaa ambavyo mtu anavitumia.

Mbwilo alisema katika mradi huo wamekuja na sera kwa Shirika la Viwango (TBS) litaenda kutengeneza viwango ambavyo majiko ya umeme yanayoingia nchini hayataingia ovyo tena.

Alisema kupitia mradi huo kuna maabara mbili ambazo zinamsaidia mwanamke anayepika aweze kujua jiko lake lina matumizi gani ili asiwe na gharama kubwa.

"Tunategemea lile wazo la Rais Samia Suluhu Hassan, la nishati safi kwa bei nafuu tunaenda kulifikia kwa sababu mradi umeangalia huo mlengo, lakini tutakuwa na kampeni kila mwananchi afahamu matumizi ya jiko ambalo halitakufanya kutumia nishati nyingi," alisema.

Mkurugenzi wa huduma za redio kutoka Shirika la Utangazaji la TBC, Aisha Dachi, alisema wanaunga mkono jitihada za wananchi kutumia nishati safi na kuachana na nishati chafu inayosababisha madhara kwa wananchi.

Alisema wamezindua kampeni hiyo itakayokuwa inatangazwa kupitia Bongo FM ya pika kijanja ambayo itakuwa endelevu kuhakikisha wananchi wanatumia nishati safi na salama.

Dachi alisema baada ya uzinduzi huo wataendelea kupitia vijijini na kufanya matamasha na kuwatafuta wadau wa nishati safi kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika katika maendeleo ya mitaji (UNCDF), Elizabeth Ngoye, alisema kuhama kutoka kwenye mkaa na kuni ni suala la taratibu kuna haja ya kuboresha sera ili kuwapo na utengenezaji bora wa mikaa na matumizi sahihi ya kuni.

Alisema wana mradi wa kutoa elimu kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupika chakula ili kupunguza madhara.



Balozi wa Kenya nchini Tanzania, Isaac Njenga (kushoto), akisalimiana na Mkuu wa Fedha wa KCB Bank Tanzania, Willis Mbatia, wakati wa mkutano wa raia wa Kenya waishio Tanzania, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Meneja wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kati wa Shirika la Ndege la Kenya (Kenya Airways), Dk. Joseph Munyeti. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Shauri la mirathi lapigwa kalenda

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Mwanzo Nzega inaendelea kupiga kalenda shauri la mirathi ya Zena Jalakhan lenye mvutano wa ndugu katika kusimamia mirathi hiyo.

Shauri hilo lililoko mbele ya Hakimu Mfawidhi, Abunas Sonyo jana liliahirishwa kwa mara nyingine hadi Aprili 23 kwa ajili ya kusikiliza pingamizi.

Mmoja wa wanafamilia, Salma Mohammed katika shauri hilo anawakilishwa na Wakili Kaumuliza David ambaye awali aliomba apewe muda wa kupitia jalada la shauri hilo la mirathi na mahakama ilikubali maombi hayo.

Jana shauri lilikuja kwa ajili ya kusikiliza mapingamizi lakini upande wa Karim Samji ambaye awali aliyekuwa kuwa msimamizi wa mirathi, uliomba shauri lisiendelee kwa sababu wakili wao hakuwapo mahakamani .

Karim alidai wakili wao hakuwapo kwa sababu hakujua mahakamani shauri linaloendelea ni lipi na baada ya mahakama kuwafahamisha kinachoendelea ni usikilizwaji wa mapingamizi, waliomba kuahirisha.

Wakili Kaumuliza aliomba mahakama iahirishe shauri hilo hadi Aprili 23, mwaka huu na hata upande wa pili walipohoji sababu za muda huo kuwa mrefu, wakili aliomba iwe tarehe hiyo kwa kuwa ndio atakuwa na nafasi.

Katika shauri hilo lenye mvutano, upande wa pili wa Salma wanapinga Karim Samji aliyeteuliwa na mahakama kusimamia mirathi ya Zena kutekeleza amri ya mahakama ya kukusanya mali za marehemu.

Salma Mohammed alifungua shauri la mirathi ya Zainabu Jalakhan kwa mali ambayo ni nyumba iliyopo pia katika mirathi ya Zena Jalakhan ambayo mahakama ilishamteua Karim kuwa msimamizi.

Mwombaji Salma aliwasilisha hoja tatu, akidai shauri linalomhusu marehemu lilikwishasikilizwa na kutolewa uamuzi katika shauri la mirathi namba 24/2023.

Hoja ya pili, mali iliyotajwa katika maombi hayo ilikwishaorodheshwa katika mirathi namba 24/2023 mbele ya Hakimu Hilda Kibona.

Katika hoja ya mwisho, shauri hilo lenye viini hivyo lilishasikilizwa na kuamuliwa na mahakama hiyo, hivyo aliomba maombi ya mirathi namba 35 ya mwaka jana ya mali ya Zena Jalakhan ambayo mahakama ilimteua Karim kuwa msimamizi yatupiliwe mbali.

Awali, mahakama hiyo mbele ya Hakimu Sonyo ilimteua Karim kuwa msimamizi wa mirathi ya mali ya marehemu Zena ambayo ni nyumba iliyopo Mtaa wa Ntinginya, wilayani Nzega, mkoani Tabora yenye namba NTC/NMSH/NTI/81.

Mahakama hiyo pia mbele ya Hakimu Hilda Kibona ilimteua Salma Mohammed kuwa msimamizi wa mirathi ya Zainabu Jalakhan ambayo nyumba iliyopo kwenye mirathi ni hiyo hiyo iliyopo Mtaa wa Ntinginya, wilayani Nzega yenye namba NTC/NMSH/NTI/81.

Hivi karibuni baada ya mahakama kufanya usuluhishi kwa familia hiyo, iliamuru aliyeteuliwa kusimamia mirathi, Karim akusanye mali za marehemu.

Hata hivyo, katika nyaraka mbalimbali za nyumba hizo ikiwamo risiti za kodi ya pango iliyowasilishwa mahakamani zinasomeka kwa jina la Zena Jalakhan na si Zainabu Jalakhan.

Karim katika kiapo chake mahakamani alidai marehemu hakuacha wosia na maelezo hayo yaliungwa mkono na wajukuu, Gullam Siager na Haji Seager, hivyo mahakama ikamteua kusimamia mirathi hiyo.

Marehemu aliacha nyumba moja iliyoko Mtaa wa Ntinginya, wilayani Nzega yenye namba NTC/NMSH/NTI/81.

Wanafamilia wanufaika katika mirathi hiyo ni wajukuu, Araf Seager, Azaz Seager, Haji Seager, Asha Seager, Gullam Seager, Fatuma Seager, Kasu Seager na Karim Samji ambaye ni mtoto.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Chanjo inayozuia malaria kwa asilimia 75 yaandaliwa

**Na Mwandishi Wetu,**
BAGAMOYO

WATAALAMU wa Taasisi ya Afya Ifakara (IHI) wako katika hatua za mwisho za utafiti wa chanjo nyingine ya malaria yenye uwezo wa kuzuia maambukizi ya ugonjwa huo kwa asilimia 75.

Mmoja wa wataalamu wa taasisi hiyo wanaoshiriki utafiti huo, Dk. Mohamed Rashid, alibainisha hayo hivi karibuni alipozungumza na waandishi wa habari waliozuru kikazi katika maabara ya taasisi hiyo wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani.

"Ni chanjo ambayo imeshafanyiwa majaribio, bado iko kwenye mwendelezo wa utafiti na matokeo yake yameonesha ina ufanisi wa asilimia 75 kulinganisha na chanjo ya kwanza tuliyozalisha.

"Chanjo ya kwanza ilikuwa na ubora kwa asilimia kati ya 36 na 40. Kwa kifupi, kuna chanjo nyingi zinajaribiwa na zinatarajiwa kuja kusaidia kukinga malaria. Ziko kwenye hatua tofauti; nyingine ya awali, nyingine ya kati na nyingine hatua ya mwisho," alisema mtaalamu huo.

Alisema chanjo ya kwanza (RTSS) waliandaa na ikapitia hatua zote hata kupata rukhsa ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kutumika kwa baadhi ya nchi kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, lakini haijaaanza kutumika nchini.

"Chanjo iliyo katika utafiti ya R21 imeonesha mafanikio makubwa, yenyewe ina ufanisi wa asilimia 75 ambayo na yenyewe pia imelenga kundi la watoto kwa sababu watoto ndio wanaoathirika zaidi.

"Kwahiyo, ni mojawapo ya chanjo za malaria ambazo zilionesha mafanikio lakini utafiti unaendelea na kuna chanjo nyingine nyingi, si moja, si mbili, si kumi zinaendelea kufanyiwa utafiti," alisema Dk. Rashid na kubainisha kuwa utafiti wa chanjo yao hiyo yenye ufanisi wa asilimia 75 ulianza mwaka 2022.

Alisema utafiti wa chanjo ya R21 uko kwenye hatua za tatu na ya mwisho, lakini haijaingia sokoni.

Alisema chanjo hupitia hatua tatu, akibainisha kuwa chanjo ya malaria ya R21 iko kwenye hatua ya tatu ambayo ni majaribio.

"Hatua ya kwanza ya chanjo inaangalia usalama wa ile chanjo. Je, ni salama? Kabla hatujajua inafanya kazi au haifanyi, tunatakiwa tujue ni salama, haina madhara kwa binadamu?

"Hatua ya pili unaangalia usalama lakini pia ufanyaji kazi, lakini hatua ya tatu inajikita zaidi katika ufanyaji kazi na usalama.

"Ile (R21) imeshafika hatua ya tatu; kwa maana imepita hatua ya kwanza ikafaulu, ikapita hatua ya pili ikafaulu, ikaenda hatua ya tatu.

"Inafanyiwa kazi vijijini huko maeneo ya Kiwangwa, Miono (Bagamoyo) ambako wanaopewa ni watoto halafu wanafuatiliwa kwa muda wa mwaka mmoja hadi miwili kuangalia je, watapata malaria au hawatapata? Hiyo ni hatua ya tatu, ni kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano," alisema.

Alibainisha kuwa utafiti huo ulitarajiwa kukamilika mwaka huu, lakini umeongezwa muda wa mwaka mmoja zaidi, hivyo utaendelea hadi mwakani, ukihusisha watoto 800.

Dk. Rashid, anayefanya utafiti wa dawa na chanjo za magonjwa mbalimbali ya kuambukiza, ikiwamo malaria, pia alishiriki utafiti wa chanjo za ugonjwa wa COVID-19.

Utafiti huo unafanyika huku takwimu zikionesha zaidi ya watoto 260,000 wenye umri chini ya miaka mitano hufariki dunia kila mwaka kutokana na malaria katika eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara.



Wataalamu wa Taasisi ya Afya Ifakara (IHI) wakieleza jambo kwa waandishi wa habari waliotembelea maabara ya taasisi hiyo Bagamoyo hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## CRB yakemea makandarasi utendaji wa kazi kwa mazoea

**Na Frank Monyo**

MSAJILI wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi Tanzania (CRB), Rhoben Nkori, amekemea tabia ya baadhi ya makandarasi kufanya kazi kwa mazoea, akiwataka kuacha tabia hiyo na bodi hiyo haitasita kufuta usajili wa kampuni zao.

Amesisitiza serikali imekuwa inatoa kipaumbele kwa miradi mingi kutekelezwa na makandarasi wazawa, lakini kuna baadhi wamekuwa wakitumia fursa hiyo kujenga taswira mbaya kwa tasnia hiyo kwa kufanya kazi bila kuzingatia weledi.

Alitoa angalizo hilo juzi Dar es Salaam alipozungumza na makandarasi zaidi ya 170 waliokuwa wanashiriki mafunzo ya siku tatu yenye lengo la kuwajengea uwezo na ujuzi wa kuandaa zabuni, kujaza mikataba, utekelezaji mikataba ya ujenzi, elimu ya kodi na kuzisimamia pamoja na kuboresha kazi zao.

"Kwa makandarasi ambao wataonekana kuchafua tasnia hii kwa kufanya kazi kwa mazoea, tunaomba ushirikiano wenu tuwaondoe kwenye usajili, wabakie wale wenye sifa zinazotakiwa na si vinginevyo.

"Matukio ya ovyo yanapotokea yanachafua tasnia na yanawaharibia ninyi nyote, wako makandarasi wengi wazuri, lakini kuendelea kupuuza wanaofanya matukio ya ovyo hawatatujengea heshima, tunaomba ushirikiano mkiwaona wanafanya hivyo msikae kimya," aliagiza.

Nkori alisema makandarasi hao wasipotoa taarifa kwa wale watakaoonekana wanafanya kazi kwa mazoea, watakuwa wanaunga mkono uovu huo, hivyo watakuwa wamejiweka katika mazingira magumu.

"Mafunzo haya lazima tuunganishe na kazi mnazofanya, kama mnahisi mnachofundishwa hamwezi kukihusianisha na shughuli mnazofanya mtakuwa mnajifedhehesha wenyewe, bodi na serikali inatumia gharama kubwa kuandaa mafunzo," alisema Nkori. Alisema serikali imejikita kutengeneza sera na mifumo rafiki ili makandarasi wa ndani wafanye kazi kwa uhuru kwa kuzingatia weledi, sheria na taratibu zilizopo; kama mkandarasi anakwenda kukopa, akope kulingana na thamani ya mradi anaotekeleza.

"Usiende kutekeleza mradi kwa kutegemea kukopa kwenye kikoba, sheria zipo lakini tunaomba makandarasi fanyeni kazi kwa weledi, kinyume cha hapo bodi haitasita kumchukulia hatua mkandarasi yeyote atakayebainika kufanya kazi kwa mazoea kwa kufutwa kwenye usajili," alionya. Alifafanua kuwa mkandarasi akifutiwa usajili hatakiwi kusajili kampuni hiyo ndani ya muda wa miaka mitatu na mmiliki wa kampuni husika hawataruhusiwa kujiunga na kampuni nyingine na ukandarasi hadi miaka miwili ipite.

"Ukiwa unafanya kazi kwenye kampuni fulani itendee haki lakini ikibainika ikafutwa kutokana na makosa ya kutokuzingatia sheria na taratibu zilizopo hamruhusiwi kusajili kampuni nyingine na kwa jina lingine hadi miaka mitatu ipite," alisema.

Msajili alisema wamiliki hawaruhusiwi kwenda kushika nafasi ya mkurugenzi kwenye kampuni yoyote ile hadi kipindi cha miaka miwili ya kutumikia adhabu ya kufutwa iishe.

## TFS kutumia 'drone' kubaini wahalifu wa misitu ya mikoko

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wilayani Kibiti, mkoani Pwani utaanza kutumia ndege picha (drone) kubaini wavamizi na waharibifu wa hifadhi ya misitu ya mikoko katika eneo hilo.

Naibu Kamishina wa Uhifadhi wa TFS, Caroline Malundo, alibainisha mpango huo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa kupokea vifaa maalum kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika hifadhi ya misitu wilayani humo kutoka Shirika la Wetland Internation. Ndege hizo zitakuwa na uwezo wa kubaini kila tukio la uhalifu msituni na kutoa taarifa.

"Kwa kutumia ndege hizi, uhalifu wowote utakaofanyika ndani ya hifadhi itakuwa na uwezo wa kubaini na kutoa taarifa kama kuna mtu anakata mti au uhalifu wa aina yoyote, itabaini na kuonesha eneo husika uhalifu huo unapofanyika.

"Na hii itatusaidia kwa kiwango kikubwa kudhibiti uhalifu ambao umekuwa tishio katika hifadhi zetu. Baada ya kubainika taarifa hizo za uhalifu, itakuwa rahisi kujipanga na hata kufaya doria kwa kwenda moja kwa moja kwenye maeneo ya tukio kuliko kwenda kutafuta pasipo kujua eneo mahsusi kama ambavyo imekuwa inafanyika," alisema Kamishina Caroline.

Alisema kuwapo mikoko kuna faida nyingi kulinganisha na misitu mingine. Hivyo, kuna haja kuongeza nguvu zaidi katika kuilinda. Mikoko inatajwa kuwa na uwezo wa kunyonya hewa ukaa mara nne zaidi ya mimea mingine.


Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Wetland Internation, Julie Mulonga, alisema wataendelea kushirikiana na TFS katika kulinda misitu asilia na kupambana na uharibifu ambao unaongezeka kila siku.

"Tuko tayari kushirikiana na TFS katika mapambano haya, uharibifu wa misitu una athari kubwa katika maisha yetu ya kila siku, hivyo hatuna budi kupambana na uharibifu unaofanywa kwa sasa," alisema Julie.

Alisema shirika hilo limepanga kutoa zaidi ya Sh. milioni 50 kwa ajili ya kuimarisha mpango mkakati wa kitaifa wa ulinzi wa mikoko Tanzania.

"Tunaamini nguvu kubwa ikiwekezwa, uhalifu wa hifadhi za misitu utapungua kama siyo kuisha na kazi hii si ya TFS peke yake, tunatakiwa kushirikiana wote kwa pamoja kwa manufaa yetu sote.

"Tumefanya kazi kwa pamoja na TFS tangu mwaka 2017 na tunaahidi kuendelea kufanya nao kazi kudumisha ushirikiano uliopo," aliahidi.



## Mapato Hifadhi ya Msitu wa Magamba yaongezeka

**Na Oscar Assenga,** LUSHOTO

WATALII wa ndani zaidi ya 4,600 wamefufua upya matumaini ya Hifadhi ya Msitu wa Mazingira Asili wa Magamba, uliopo Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga, mapato yake kupanda maradufu kutokana na shughuli za utalii.

Ongezeko hilo ni sawa na wageni 800 kwa mwaka 2023, ukilinganisha na wageni waliotembelea mwaka 2022.

Mhifadhi Mkuu wa Msitu wa Mazingira Asili wa Magamba, Christoganus Vyokuta, alitoa takwimu hizo jana wakati wa kikao chake na wadau wa usafirishaji wa pikipiki, maarufu kama bodaboda.

"Hivi sasa takwimu zimekuwa zikipanda na kwa mwaka huu wa fedha unaomalizika, watalii zaidi ya 4,600 waliitembelea hifadhi yetu, ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita, ambapo waliitembelea wageni 3,800.

"Ukiangalia takwimu hizo, utaona Watanzania wengi wamehamasisha kuja kutembelea eneo hili la kivutio cha asili cha Magamba; na inaleta hamasa kwa Watanzania wengi kuona bora kutumia vivutio hivyo."

Magamba ni hifadhi tofauti na nyingine za asili, ambapo yenyewe pia ina vivutio vya kihistoria ikiwamo jengo la ofisi za kale, handaki lililotumiwa na Wajerumani na jiwe lenye historia ya aina yake.

Ili kuvutia zaidi utalii wake, menejimenti ya hifadhi hiyo, imeamua kuanza kuwatumia waendesha bodaboda kuvuta watalii, baada ya kuwatumia kujitangaza kwa maandishi yenye ujumbe murua wa 'Ask me about Magamba'

Kutokana na hamasa hiyo, menejimenti ya hifadhi hiyo imekutana na waendesha bodaboda 50 na kuingia makubaliano ya kutangaza utalii wa Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Magamba.

# Hospitali za KKKT kufanya uchunguzi saratani matiti bure

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

HOSPITALI tatu zinazomilikiwa na Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), zimetangaza kuanza rasmi kampeni ya uchunguzi wa saratani ya matiti, kwa wanawake wenye umri kati ya miaka 25 hadi 70.

Uchunguzi huo utakaoongozwa na jopo la madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC, utafanyika kwa siku tofauti katika Hospitali Teule ya Machame iliyoko Wilaya ya Hai na Hospitali ya Marangu ya Kitemboni (Kilimanjaro), na Hospitali ya Wilaya ya Karatu (Arusha).

Jana, Katibu wa Afya wa Dayosisi ya Kaskazini, Joshua Ndaga, alisema uchunguzi huo unafanyika kutokana na wito au moyo wa huruma alioupata Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, Dk. Fredrick Shoo.

Alisema Askofu Dk. Shoo, ameguswa na ongezeko la idadi ya wanawake wenye changamoto ya saratani ya matiti na kuaamua kutafuta fedha za kuwezesha kampeni hiyo kufanyika.

Saratani ya matiti ni mabadiliko ya chembechembe hai zilizopo kwenye matiti, saratani hii kwa kawaida haina dalili katika hatua za mwanzo.

Wanawake katika hatua za mwanzo za ugonjwa huo, hawana maumivu au dalili nyingine zozote.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, uchunguzi wa awali, ndiyo ambao huwezesha kuugundua ugonjwa katika hatua ya mabadiliko yaletwayo na saratani ya matiti.

Vilevile, Ndaga, ameeleza zaidi kuwa baadhi ya wanawake hushindwa kuigundua mapema na kupata msaada na wengine, wakidhani kuwa wamepata jipu katika matiti.

Kutokana na madhara ya ugonjwa huo, Ndaga, amewasihi wanawake wote wanaoweza kuzifikia hospitali hizo kujitokeza kwa wingi kupata huduma hiyo, kwa kuzingatia tarehe zilizopangwa kwa kila hospitali na huduma hiyo itatolewa bure.

"Huduma hiyo, ambayo itafanywa kwa kushirikiana na madaktari kutoka Hospitali ya Rufaa ya Kanda KCMC, imepangwa kufanyika katika Hospitali za Karatu, Machame na Marangu. Huduma itatolewa katika Hospitali ya Wiaya ya Karatu, Machi 19 na 20 mwaka huu.

Katika Hospitali ya Machame, uchunguzi huo utafanyika Machi 22 na 23 mwaka huu. Wakati katika Hospitali ya Marangu, uchunguzi huo utafanyika Aprili 4 na 5 mwaka huu.

Alipotafutwa na Nipashe kuzungumziaa makali ya ugonjwa huo, Daktari Bingwa wa magonjwa ya saratani wa KCMC, Furaha Servent, alisema ripoti za utafiti wa ugonjwa huo zinaonyesha kuna dalili idadi ya wagonjwa wa saratani, kuongezeka mara mbili ya sasa ifikapo mwaka 2030.

Aidha, alisema asilimia 95 ya magonjwa ya saratani yanatokana na mtindo wa maisha, ikiwemo ulaji mbaya wa vyakula, na asilimia 15 inatokana na kurithi.



Mkuu wa Wilaya ya Mkinga mteule, Kanali Evance Mtambi, akila kiapo mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dk. Batilda Buriani jana, baada ya uteuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan. Kushoto ni Katibu Tawala wa Mkoa huo, Pili Mnyema. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Wizara yashauriwa kuanzisha kampeni ujumuishwaji maamuzi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SHIRIKA la Voice Of Empowed Women (VOEWOF), limeishauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, kuja na kampeni maalum ya kuhamasisha suala la ujumuishwaji katika kila ngazi ya maamuzi, kuanzia kwenye familia hadi serikalini.

Aidha, limewataka Watanzania kuelewa kuwa hakuna ujumuishwaji wa mwanamke peke yake, huku likiwataka kuondoa dhana hiyo ili kufikia maendeleo.

Mkurugenzi wa VOEWOF, Asifiwe Mallya, aliyasema hayo wakati akizungumza na makundi maalum katika Kata ya Boman'gombe, Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro.

Alisema bado wanajamii wana ukakasi katika suala la ujumuishaji, hivyo kundi moja kuendelea kukosa uwakilishi sahihi.

Asifiwe alikuwa akiteta na watu wenye ulemavu, wanawake, vijana na watoto, kama sehemu ya shirika hilo kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani.

"Ujumuishaji unasaidia kuondoa unyanyapaa, inaondoa ujinga, kutengwa hasa kwa jamii ya watu wenye ulemavu. Kwa hiyo ni muhimu kwa wizara husika kuja na mkakati maalum wa kutoa elimu kuhusiana na ajenda hii.


...Uwekezaji ni mchakato na ili ufanikiwe, ni lazima mwanamke ajumuishwe na ahusishwe katika mchakato mzima. Hata hivyo, maaendeleo endelevu yanakuwa na maana pale ambapo hakuna watu au kundi la watu linaachwa nyuma. Tunajadili mambo muhimu ambayo yatakuwa na mchango muhimu katika Dira ya Taifa ya Mwaka 2050."

Zaidi aliongeza: "Kwa hiyo hatuwezi tukasema tunaakuwa na maendeleo endelevu kama tutakuwa tunaacha makundi mengine nyuma. Tumehakikisha kila kundi limewakilisha katika mjadala wetu wa uchechemuzi wa Siku ya Wanawake Duniani. Tumejumuisha wanawake, watoto, jaamii za kifugaji, watu wenye ulemavu na baadhi ya wanaume waliotuunga mkono."

Mkurugenzi wa Shirika la Ability & Disability in Tanzania, William Kivuyo, ambaye pia Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya Emilia, alisema lengo lao ni kuonyesha kwamba kila mtoto mwenye ulemavu au anayeishi na ulemavu anapata huduma zote za kiafya kuweza kuimarisha mahusiano.

Alisema: "Tunafanya hivyo kwa kuwawezesha na kuungana na wawezeshaji wengine katika shule na kanisa, hospitali na jamii kwa ajili ya kuweka wigo mpana wa kuwasaidia wenye ulemavu au watoto wenye ulemavu ambao wanakosa huduma hizo za kuboresha maisha yao.

"Malengo yetu ni kuwatafuta na kuwabainisha walipo hao watoto wenye ulemavu, halafu la pili ni kuwaunganisha na familia katika huduma za afya, tiba za utengemao, elimu na stadi za ufundi ili kuweza kujikimu katika maisha."





# Wanafunzi 813 wakacha kuripoti shuleni, msako watangazwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WENYEVITI wa vijiji pamoja na watendaji wa kata katika Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wamepewa jukumu la kuwasaka wanafunzi 813 kati ya 5,757 walichaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu, lakini hawajulikani walipo.

Agizo hilo limetolewa juzi na Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji wa Halmashauri hiyo, Doa Limbu, wakati wa kikao cha tathmini ya matokeo ya darasa la nne na saba na kutaja viongozi hao kuwa suluhu ya tatizo hilo.

Limbu ambaye ni Diwani wa Nyankende, alisema kati ya wanafunzi 5,757 walichaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu ni wanafunzi 4,851 wamefanikiwa kuripoti, huku 813 wametokomea kusiko julikana. Limbu alisema serikali za vijiji zinawajibika kuwatafuta wanafunzi hao na kuwapeleka shuleni.

"Kwa kuwa orodha ya majina yao tunayo ni kwenda moja kwa moja kwenye kaya zao na kuwarejesha shuleni na tukikuta mwanafunzi hayupo mzazi wake ajiandae kutupatia majibu ya kutosha kuhusu mahali alipo mtoto huyo," alisema Limbu.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Charahani alisema wakuu wa shule za sekondari tayari wamepeleka orodha ya wanafunzi ambao ambao hawajaripoti shuleni katika ofisa za watendaji wa vijiji na kata, lakini mpaka sasa hakuna hatua zilizochukuliwa kwa wazazi waliobaki na wanafunzi hao.

Alidai kuwa watendaji hao wamekuwa wakiwaita wazazi ofisini lakini mwisho wake wanaishia kumalizana na hakuna mrejesho kwa walimu wakuu juu ya hatua zinazochukuliwa.

Hivyo alimshauri Mkurugenzi Hadija Kabojela kuwaita watendaji kata wote na kuwabana juu ya wanafunzi hao, kuhakikisha wanapatikana.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Hadija Kabojela aliahidi kuwaita kwa pamoja watendaji hao na kujadili namna ya kuwapata wanafunzi hao na kusema kwa wazazi waliongia tamaa ya kuwaozesha wajiandae kuwajibishwa kisheria.




Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Juma Chikoka (wa pili kushoto), akizungumza katika mahafali ya mafunzo ya programu ya maendeleo ya kibiashara ya Barrick North Mara, yaliyomalizika katika mgodi huo, wilayani Tarime jana, yaliyolenga kuimarisha uwezo wa biashara za ndani ili ziweze kunufaika na fursa zilizopo kwenye sekta ya madini. Wawakilishi kutoka kampuni 19 za wazawa wilayani humo walihitimu mafunzo hayo ya miezi sita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# LATRA yanasa maboksi 100 ya tiketi zilizopigwa marufuku

**Na Benny Kingson,** TABORA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) Mkoa wa Tabora limekamata boksi zaidi ya 100 zenye vitabu vya tiketi ambazo zimepigwa marufuku kutumika.

Tiketi hizo zilikuwa zikiendelea kutumiwa na baadhi ya mawakala wa mabasi kwa kuwapandishia nauli abiria kinyume cha sheria. Ofisa Mfawidhi wa LATRA mkoani hapa, Nelson Mmari, alibainisha hayo akiongea na Nipashe ofisini kwake na kutaja ukamataji wa boksi hizo umefanyika baada ya operesheni wanayoendelea kuifanya katika ukaguzi wa shughuli zote za usafirishaji iliyobaini mambo mengi yanayofanyika kinyume na utaratibu.

Mmari alisema licha ya kuhamasisha matumizi ya tiketi mtandao ili kudhibiti ukwepaji kodi pamoja na kuzuia matumizi ya vitabu, kuwaondolea usumbufu abiria wa kulipa nauli zaidi kwa kutapeliwa na mawakala wasiokuwa waaminifu lakini vitabu hivyo vimeendelea kutumika kwa uficho na kuwaumiza abiria.

"Katika msako huo pia tulibaini abiria mmoja kutozwa nauli zaidi toka Tabora kwenda Manyoni mkoani Singida ambapo badala ya kutozwa Sh.13,000 alitozwa Sh.40,000 ikiwa ni tofauti ya Sh. 27,000.

Alisema kuwa mawakala wamekuwa na tabia ya kuwakatia abiria tiketi zisizotakiwa kwa kuwatoza nauli kubwa kinyume na bei elekezi, lakini pindi mabasi yanapokaribia kuondoka uwafuata abiria na kuchukua tiketi hizo na kuwapa tiketi mtandao zenye gharama inayokubalika na hivyo kupoteza ushahidi wa maovu yao.

Pia alisema yapo magari madogo 'daladala' yanazotoza nauli kubwa kinyume na ile iliyopangwa na serikali ambapo eneo la kulipa Sh.2,000 wanalazimika kulipa Sh. 3,000.

Kuhusu tatizo la wapigadebe katika vituo vya mabasi, Mmari alisema walikaa kikao na Mkurugenzi pamoja na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo Dk. Betilda Buriani.

Alisema katika kikao hicho, Buriani alimwagiza Mkurugenzi kukutana na timu yake kuanda vitambulisho vya kuwapa mawakala wa mabasi na watumishi wao ambao watakuwa wanaingia kituoni na kutambulika rasmi.

## Mgodi wa dhahabu wadaiwa kuendeshwa bila vyoo

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

MGODI wa Dhahabu Chapakazi uliopo katika Kijiji cha Wisolele Kata ya Segese wilayani Kahama mkoani Shinyanga, umetajwa kuendesha shughuli zake bila kuwa na vyoo, hali inayohatarisha afya na usalama wa wachimbaji.

Nipashe ilitembelea mgodi huo juzi na kushuhudia kutokuwapo kwa vyoo katika maeneo hayo, huku baadhi ya wasimamizi wake wakiwaelekeza wageni wanaofika hapo kwenda kujisaidia vichakani.

Mmoja wa wachimbaji mgodini hapo aliyeomba jina lake lihifadhiwe alisema ni kwa kipindi kirefu mgodini hapo hakuna huduma ya vyoo na pindi wanapotaka kujisaidia wamekuwa wakienda vichakani hali ambayo ni hatari kiafya.

Msimamizi wa usalama mgodini hapo, Edward Herman, alisema barua kuhusu maelekezo yaliyotolewa na serikali waliipata hivi karibuni kwa kuchelewa na kwamba pamoja na kupita kwa siku 14 zilizotolewa lakini hawajapuuza utekelezaji wake kwa vile tayari wameanza kufanyia kazi yaliyoelekezwa.

"Juzi tulikuwa na timu ya wakaguzi kutoka wizarani ambao wamekagua eneo letu lote na sasa tunasubiri maelekezo yao pia, tulianza uchimbaji wa shimo la choo lakini wachimbaji walikumbana na mwamba wa jiwe la dhahabu hivyo kusitisha shughuli hizo kwanza," alisema Herman.

Ofisa Madini wa mkoa wa kimadini Kahama, Joseph Kumburu, alipoulizwa juu ya hatua zilizochukuliwa dhidi ya migodi ambayo haijatekeleza agizo hilo alisema tayari kuna timu ya kufuatilia utekelezaji wa maelekezo hayo katika maeneo yote ya migodi ili kuona kama kilichoagizwa kimetekelezwa na kuwachukulia sheria wote wasiofuata utaratibu.

Kwa mujibu wa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, juzi katika kikao cha RCC alitaja Mkoa wa Shinyanga kuwa bado unakabiliwa ugonjwa wa kipindupindu katika baadhi ya wilaya.

Alisema tayari wagonjwa 216 wameripotiwa huku 127 wakibainika kuwa na kipindupindu.

Kutokana na hali hiyo, Mndeme aliwaagiza maofisa afya wote mkoani humo kuhakikisha maeneo yote yenye mikusanyiko ya watu, kila nyumba na sehemu za shughuli za kijamii inawekwa huduma ya maji tiririka kwa ajili ya watu kunawa mikono.



Ukurasa 12

**Uwekezaji kwa wanawake ulivyo ajenda ya kudumu**



Ukurasa 13

**ILANI YA UCHAGUZI YA WANAWAKE...**
Wanasiasa wanaotoa ahadi hewa hawana la kuwapa wapigakura



Ukurasa 14

**Baada ya kuishi ikulu miaka 30 bado anaamini pekee ana hati miliki urais**


# siasa

JUMATANO MACHI 13, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


PANGA PANGUA YA RAIS

# Cheche za Makonda zilivyokula vichwa viongozi wasiowajibika

**Na Beatrice Shayo**

ZIARA ya Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, imeanza kutembeza fagio la chuma kwa baadhi ya watendaji na viongozi wanaodaiwa kuwa 'wanazingua.'

Katika moja ya maonyo yake Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akizungumza kwa utani akiwaambia viongozi 'ukinizingua na mimi nitakuzingua,' akimaanisha hatamvumilia mtu asiyetekeleza majukumu ya kuhudumia wananchi.

Mwishoni mwa wiki Rais, alifanya mabadiliko madogo ya wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri, akiwahamisha, kuwaondoa na kuteua wapya.

Mabadiliko hayo yanajiri mwezi mmoja baada ya ziara ya Mwenezi Makonda katika mikoa 23 alikofanya mikutano 247 na kusikiliza kero zaidi ya 2,009. Kabla ya kuhitimisha ziara, Makonda anaahidi atawasilisha ripoti kwa Rais Samia, kuhusu viongozi wazembe baada ya kukuta wananchi wanateseka kupata haki zao.

"Nilisema kilichopatikana kwa maombi hakifi kwa majungu, wale ambao hamfanyi kazi siku ukiona umebadilishwa au umetenguliwa kwenye maeneo niliyopita usimlamu Rais, Makamu wa Rais, Philip Mpango wala Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa nilaumu mimi," anasisitiza Makonda.

Akiwa katika ziara mikoani, Makonda anaeleza kuwa matatizo mengi ya wananchi yanasababishwa na viongozi kutowajibika.

Aidha, tathmini ya ziara yake inabaini kukithiri dhuluma sekta ya ardhi inayohusisha wenye fedha wanaoshirikiana na watumishi wa umma dhidi ya maskini, mambo aliyosema yanasababisha wananchi kuichukia serikali.



Dk. Francis Michael aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe, uteuzi wake umetenguliwa na nafasi yake imechukuliwa na Daniel Chongolo. **PICHA: MTANDAO**

"Kubwa tulilolibaini ni Watanzania wengi kuumizwa na dhuluma, iliyogawanyika katika maeneo mengi au kwenye sekta nyingi na chama tuna wajibu wa kuweka mkazo wa kupambana nayo."

Kauli ya Makonda imetimia baada ya baadhi ya maeneo ambayo yamelalamikiwa mabadiliko ya viongozi kufanyika.

Mkoani Iringa, malalamiko mengi yaliyotolewa na wananchi ni kuwapo kwa migogoro ya ardhi inayodaiwa kusababishwa na watumishi wa idara hiyo. Panga pangua, iliyotokea imemgusa Mkuu wa Mkoa, Halima Dendego, aliyehamishiwa Singida, pia Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Veronica Kessy, aliyepelekwa Bumbuli.

Wananchi walimtuhumu mbele ya Makonda, Mthamini Ardhi Mkoa, Priscus Shirima, kuhusika na migogoro mingi, huku fedha zikidaiwa kutumika kupora maeneo yao. Akiwa Iringa Makonda alimuuliza Dendegu kuwepo utitiri wa migogoro, mkuu wa mkoa akimjibu kuwa amepambana sana katika hilo jambo.

"Migogoro ya ardhi kibao namuuliza dada yangu Halima Dendegu ananiambia kaka hapa nimepambana kakuta watumishi wapo wana miaka 20 badala ya kuwa sehemu ya msaada wamekuwa madalali wa viwanja," anasema Makonda.

Peter Serukamba Mkuu wa Mkoa wa Singida, amepelekwa Iringa wakati Mkuu wa Wilaya ya Singida, Paskasi Muragili, amekuwa Mkuu wa Wilaya ya Bukombe katika mabadiliko hayo yaliyowagusa wote wawili.

Waliotoa kero kwa Makonda mkoani humo walilalamikia matatizo ya ardhi pamoja na mikopo ya kausha damu inayowatesa hasa wanawake. Pangua hiyo haikumwacha salama Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba, ambaye amepelekwa Halmashauri ya Lindi.

Huyu, alilamikiwa na wananchi kuwa ni chanzo cha migogoro ya ardhi katika manispaa hiyo akilaumiwa kukosa ushirikiano na kutoa majibu mabaya.

Aidha, wananchi walimzomea Msumba wakidai anafanya kazi kwa mazoea kwa sababu ya kuwapo Kahama kwa miaka mingi.

Aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tanga, Said Majaliwa, amehamishiwa Halmashauri ya Mji wa Kondoa.

Akiwa Tanga Makonda, alikutana na kilio cha mwanaCCM Nassor Fereji, cha kuporwa nyumba na kiongozi wa chama hicho.

"Niliombwa nyumba na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Tanga Mjini, Khamis Mkoba, kwa sababu ipo jirani na ofisi ya chama ili wawaweke makatibu. Nilikubali kwa sababu ni mwanachama pia na ninaipenda CCM," analalamika Fereji mbele ya Makonda.

Anasema alitoa nyumba yake yenye hati za umiliki, aliyouziwa na mmiliki wa kwanza, lakini hadi sasa ameporwa na akiuliza anajibiwa kuwa hana chake, jambo lililomshangaza. Makonda aliagiza kiongozi huyo wa CCM kuirejesha nyumba hiyo mara moja kwa Fereji na kuonya kuwa alichofanya si tabia ya CCM bali ni yake binafsi.

Tanga ni mkoa ambao Makonda alisikiliza kero za wananchi na kupokea migogoro mingi ya ardhi, akiwataka viongozi hao kufungua ofisi Jumapili asubuhi kutatua matatizo ya wananchi kwa kuwa wameshindwa kuwajibika katika siku za kazi.

"Migogoro mingi ya ardhi niliyokutana nayo ni kutowajibika kwa watendaji endapo wangewajibika nisingepokea malalamiko mengi ya wananchi. Acheni kuchati ofisini badala yake wasikilizeni na kutatua kero za wananchi." Anaagiza.

**INAENDELEA UK. 14**

# Uwekezaji kwa wanawake ulivyo ajenda ya kudumu



Doroth Semu, baada ya kuwa Makamu Mwenyekiti-Bara, amechaguliwa kuwa Kiongozi wa Chama cha ACT- Wazalendo, akichukua nafasi ya mwasisi Zitto Kabwe. ACT-Wazalendo inaonyesha mfano wa uwekezaji kwenye uongozi wa wanawake kisiasa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Dk. Reubeni Lumbagala,**

**DODOMA**

UWEKEZAJI kwa mwanamke, kuharakisha maendeleo ya taifa na ustawi wa jamii ndiyo kaulimbiu ya Siku ya Mwanamke Duniani mwaka 2024.

Ikumbukwe Machi 8, kila mwaka dunia huadhimisha siku ya wanawake, ambao ni wasaa kwa 'jeshi kubwa' katika ngazi mbalimbali kujadili mustakabali wa maendeleo yao, mafanikio, changamoto na nini kifanyike ili kumwinua mama na binti katika nyanja za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Kauli mbiu hiyo ni rai ya wadau wanaotetea haki za wanawake kuhimiza umuhimu wa familia, jamii, AZAKI na serikali kuwekeza kwa wanawake kwani ndiyo uwekezaji wenye mchango wa moja kwa moja wa kuharakisha maendeleo ya taifa na ustawi wa jamii nzima.

Tanzania inatambua umuhimu wa mwanamke katika kufanikisha kufikia maendeleo, ndiyo maana katika alama mojawapo inayolitambulisha taifa hili ni nembo yenye picha ya mwanamume na mwanamke.

> Kuwainua kuanzie kwa watoto, mabinti ili nguvu ya pamoja ya wanaume na wanawake iweze kuzaa matunda ya maendeleo endelevu.

Tafsiri yake ni kuwa ili kufikia maendeleo ya kweli, ni lazima kuunganisha juhudi za pamoja za mwanamume na mwanawake au kuwa na usawa wa kijinsia katika hatua zote zinazohusu kumwondoa maskini mwanamke katika hali duni na kumpa hali bora zaidi.

Hakuna namna ambayo mipango, mikakati na malengo ya familia, jamii na taifa lolote yanaweza kufikiwa kikamilifu kama wasichana na wanawake wataachwa nyuma bila kushirikishwa ipasavyo.

Kutokana na ukweli huo kuhusu umuhimu wa ushirikishwaji wa wanawake katika kuharakisha juhudi za kufikia maendeleo, ni lazima kila mmoja kuona na kukifanya kipaumbele kumwinua mwanamke.

Kuwainua kuanzie kwa watoto, mabinti ili nguvu ya pamoja ya wanaume na wanawake iweze kuzaa matunda ya maendeleo endelevu.

Familia ni taasisi ya kwanza ambayo ikifanikiwa kwenye uwekezaji kwa wasichana na wanawake, taifa linapiga hatua kubwa za kimaendeleo kwa haraka zaidi.

Wazazi (baba na mama) na walezi ambao ni viongozi katika familia wanalo jukumu la kuwapa nafasi watoto wa kike kupata elimu kwani ndiyo uwekezaji na urithi mkubwa kwao.

Hivyo, wanatakiwa kuwa na utashi wa kutoa fursa sawa za kielimu kwa watoto wao wakike na wakiume, ukombozi katika familia hizo utakuwa ni wa uhakika kwani watoto wote wa kiume na wa kike watachangia maendeleo ya familia zao na kuzikomboa katika changamoto mbalimbali.

Kuwekeza kwa wasichana badala ya kuwaoza ili kupata mahari ambayo ni fedha na mifugo, wazazi na walezi waachane na tabia ya kunyanyasa watoto wa kike katika umri mdogo kwa kuwaingiza kwenye ndoa za utotoni.

Ikumbukwe kuwaoza ni kuwakatisha ndoto zao, waachwe wafikie ndoto walizonazo na hivyo kutoa mchango katika juhudi za kufikia maendeleo.

Wakumbuke kuwa ndoa za utotoni ni adui wa uwekezaji kwa wasichana kwani zinafifisha mipango na maono ya wasichana hasa vijijini.

Jamii kwa sehemu yao wanayo nafasi ya kuchangia uwekezaji kwa wanawake ili kupata maendeleo na usawa kijinsia.

Jamii inapaswa kuunga mkono mipango ya kuwainua wasichana na wanawake badala ya kuwa sehemu ya kukwamisha mipango ya maendeleo. Vilevile, ndiyo inayopaswa kukemea viashiria na vitendo vyote vyenye lengo ya kurudisha nyuma ukombozi wa wasichana na wanawake.

Jamii yenye mdomo mpana ikiunga mkono juhudi za ukombozi wa wasichana na wanawake, ni nani anaweza kuzuia na kurudisha nyuma ukombozi wa mwanawake?

Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, imeonyesha utashi wa kisiasa kuhakikisha ukombozi wa wasichana na wanawake unafikiwa kikamilifu ili kuharakisha juhudi za maendeleo.

Kwa upande wa elimu, serikali imetoa fursa kwa watoto wa kike wanaopata changamoto mbalimbali kuanzia ujauzito, maradhi na ukata wa familia kuendelea na masomo ili yote yanayowakwamisha yasiwe kikwazo cha kufikia ndoto walizonazo katika maisha yao kupitia elimu.

Uwekezaji kwenye sekta ya elimu uliopelekea ongezeko la taasisi mbalimbali za elimu kuanzia shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vikuu, kunaongeza fursa kwa wasichana kupata elimu na hivyo kuchochea juhudi za ukombozi kwa wanawake.

Kiuchumi, serikali imeongeza kasi ya uwezeshaji wanawake mathalani kutoa mikopo ili kuwasaidia wanawake kushiriki katika shughuli za kiuchumi, na uwekezaji licha ya kwamba mikopo ya halmashauri ya 4:4:2 asilimia 4 wanawake, 4 vijana na 2 wenye ulemavu, uboreshaji ukopeshaji ukikamilika kazi itaendelea.

Ukombozi wa mwanamke kwenye nishati ni ajenda ambayo serikali ya Rais Samia inaibeba, kwa mfano mikakati ya kuachana na kuni na mkaa inaendelea huku matumizi ya gesi na umeme ukihimizwa.

Kisiasa, wasichana na wanawake wamehimizwa kuthubutu na kujitokeza kugombea nafsi mbalimbali za uongozi ili kuwa na nafasi za maamuzi na hivyo kuharakisha uwasilishaji wa mikakati inayowanufaisha wanawake moja kwa moja.

Wanawake walioaminiwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi, wameonyesha uwezo mkubwa wa kiuongozi na hivyo kuthibitisha kuwa wanawake wanaweza uongozi. Ili nchi hii iendelee kupiga hatua za kimaendeleo kwa kasi kubwa, ni lazima uwekezaji kwa wasichana na wanawake uongezeke mara dufu.

Hili likiendelea kufanyika kwa kasi kubwa, Tanzania itapiga hatua kubwa zaidi za kimaendeleo katika kipindi kifupi.

***Mwandishi ni mwalimu wa Mlali Sekondari iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***
***Maoni: 0620 800 462.***

ILANI YA UCHAGUZI YA WANAWAKE...

# Wanasiasa wanaotoa ahadi hewa hawana la kuwapa wapigakura

## • Wanawake wazipangue na kuwapuuza matapeli

**Na Gaudensia Mngumi**

KWENYE moja ya kampeni za uchaguzi mkuu, mgombea anaahidi kujenga daraja na kuapa kwa miungu yote kuwa kama halitajengwa akatwe kidole gumba.

Baada ya miaka mitano, anarudi tena kuomba kuchaguliwa aongoze jimbo. Anashangaa kukutana na mabango yenye mapanga na visu.

Hakukumbuka alichoahidi hadi aliposoma 'tunakukata kidole liko wapi daraja letu?'

Ndiyo mfano wa ahadi hewa, wagombea au watiania wanazowahadaa wapigakura ili wawachague kwenye uongozi.

Ni ujumbe kwa wanasiasa wanaotangaza nia ya kuwania uongozi iwe kwenye serikali za mitaa au ubunge ama udiwani na urais kwenye chaguzi zinazoanza mwaka huu.

Wanaonywa na Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake, inayoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) Mtandao wa Wanawake na Katiba kwa udhamini wa Mfuko wa Udhamini wa Wanawake (WFT-T).

Ilani inaangazia uchaguzi wa serikali za mitaa na mkuu wa 2025.

Ilani inawaonya wanaotoa ahadi hewa kuwa wanaozitoa hawana kipya cha kuwafanyia wananchi badala yake wanawadanganya.

Aidha, inawataka wapigakura kuwa makini na wagombea hao na kuwataka waonyeshe nia na njia za dhati za kuleta usawa wa kijinsia na kuyapa kipaumbele masuala kama ukatili na ubaguzi wa kijinsia na namna watakavyoyaondoa.

### UJUMBE WA VYAMA

Vyama vya siasa vinatajwa na ilani kuwa ni walinzi wa lango kuu la kuingia katika kinyang'anyiro cha uchaguzi na kwenye nafasi za uongozi kitaifa, hivyo inazidai mengi taasisi hizo.

Mosi, inavitaka kuchukua hatua za kuchagua na kuteua viongozi ndani ya vyama ili kutoa fursa kwa wanachama wanawake kushiriki katika uongozi na uamuzi ndani ya chama.

Aidha, vizingatie misingi iliyobainishwa kwenye mikataba ya kimataifa, kikanda, katiba ya Tanzania na dira ya 2025 kuhusu usawa wa kijinsia kwenye uongozi ndani ya vyama hivyo.

Kadhalika vyama vijielimishe kuhusu faida za kuzingatia usawa wa jinsia katika uongozi na maamuzi ndani ya taasisi hizo ili kuujua umuhimu wa kuleta mabadiliko katika mfumo wa uongozi ndani ya taasisi hizo.

Halikadhalika, vyama hivyo vitenge mafungu maalumu kuwawezesha wanawake vijana kushiriki katika uongozi, lakini viache malumbano ya ubinafsi badala yake vijenge hoja na utamaduni wa majadiliano ya kistaarabu yasiyo na vitisho au vitendo vya kuwadhalilisha wakati wa mchakato wa uchaguzi.




Mkurugenzi wa Chama cha Wanahabari Wanawake TAMWA –Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, akizungumzia umuhimu wa kuweka taswira chanya ya mwanamke katika vyombo vya habari na harakati za maendeleo. **PICHA: TAMWA**

Pia inavitaka vionyeshe nia ya kupambana na ufisadi na rushwa za aina zote ikiwamo ya ngono kwa wagombea wanawake na ukatili wa kingono dhidi yao.

Ilani inavionya viache kutumia viti maalumu kushawishi wanawake kujiondoa kwenye nafasi za kushindana majimboni, jambo linalosababisha kuwatumia kuwapigia debe wanaume wanaowania nafasi hizo.

"Wanawake wanachama wa vyama vya siasa watambue kwamba wanapochaguliwa kwa mfumo wa 'viti maalumu' hawana fursa sawa za ushiriki. Hawawezi kuteuliwa kwenye nafasi ya Waziri Mkuu au katika mabaraza ya mikoa," inaonya ilani.

Inaeleza kuwa walioingia kwa mfumo wa viti maalumu hubaguliwa katika uteuzi wa wenye viti wa kamati mbalimbali hata kama sheria hazikatazi.

Kadhalika, hawapati fedha za mfuko wa maendeleo ya jimbo zinazowawezesha wabunge waliochaguliwa kwa kura majimboni kuendelea kujiimarisha kwenye uchaguzi.

### HAWATAUNGA MKONO

Kwa kauli zao ndani ya ilani wanawake, wanasema hawatakuunga mkono chama kisichoonyesha nia ya kubomoa mfumo dume na mifumo kandamizi ndani ya vyama.

Mifumo hiyo inajidhihirisha kwenye safu za uongozi ndani ya vyama na ile ya waliojitolea kuwania nafasi kwenye chaguzi za serikali na mitaa na uchaguzi mkuu wa 2025.

"Chama chenye uongozi unaodhalilisha wanawake katika ngazi yoyote kuanzia kwenye kaya, hakitaungwa mkono. Hata vyama au chama chenye historia ya kufuja mali za taifa na kujilimbikizia mali kwa njia zisizo halali."

Vilevile hakuna kuunga mkono vyama visivyoonyesha utayari wa kimkakati wa kufungua milango ili wanawake washiriki kikamilifu ndani ya vyama vyao na katika kuwania uongozi wakati wa uchaguzi.

"Sisi wanamtandao wa wanawake, katiba, uongozi na uchaguzi pamoja na mitandao mingine ya tapo (movement) la ukombozi wa wanawake kwa sauti moja tunakiri tutaunga mkono vyama vilivyoteua wagombea katika nafasi mbalimbali ambao kwa maoni yetu ni wagombea wenye kuheshimu utu wa wanawake.

Wasio na tamaa ya kuhodhi mamlaka, walio tayari kusimamia na kuweka mbele maslahi ya taifa ili rasilimali au utajiri wa Tanzania unatumika kwa manufaa ya wote."

Aidha, inasema wagombea ambao hawana historia ya ufujaji, wizi na hata kashfa za ngono na udhalilishaji wowote wa kijinisia, wataungwa mkono pia.

> Chama chenye uongozi unaodhalilisha wanawake katika ngazi yoyote kuanzia kwenye kaya, hakitaungwa mkono.

### KUNUNUA KURA

Ilani inasema katika chaguzi zilizopita wanaharakati wapigakura walishuhudia wagombea wasio na sifa wakihaha kutumia uwezo wao kifedha kununua kura.

Inamfananisha kiongozi huyo na sumu kwa taifa, maendeleo ya demokrasia na hata kwa harakati zinazolenga kuwakomboa wanawake na makundi yaliyo pembezoni yanayotaabika kutokana na rasilimali za taifa kutowafikia.

"Vile vile tulishuhudia wagombea wakitumia lugha ya kuwadhalilisha wagombea wengine hasa wanawake. Kwa umoja wetu tunasema anayetumia lugha ya kudhalilisha utu wa mwanamke amefilisika kimawazo tena asiyestahili kura zetu."

Ilani inawaonya wagombea wasitumie nguvu ya fedha kununua kura bali busara na nguvu ya hoja kushawishi wapigakura. Pia mgombea au mpigadebe anatakiwa ajiepushe na kutumia matusi au ubabe kudhalilisha wanawake wagombea.

### ASASI ZA KIRAIA

Ilani inaeleza kuwa katika ilani zilizopita asasi nyingi za kiraia zimejihusisha na elimu ya mpigakura ikiwa ni pamoja na kuhamasisha kupigakura, kuwachagua viongozi bora na waadilifu.

Aidha, elimu ya wapigakura imetolewa siku chache kabla ya uchaguzi na haikuwa endelevu kuna asasi chache sana zilizowekeza kwenye kutetea na kuhamasisha jamii kuhimiza wanawake wenye uwezo kujitokeza zipo chache zilizowezesha kwa njia ya elimu na zilizoendeleza elimu ya wapigakura kwa muda mrefu ni chache.

Ilani inaeleza kuwa kasoro hiyo inaathiri uelewa wa wapigakura kuhusu kanuni, taratibu na haki na wajibu wao katika uchaguzi wa viongozi.

Inazitaka kuunganisha nguvu ya pamoja katika kuhamasisha wanawake wenye uwezo kugombea nafasi za uongozi kukataa kuburuzwa kama wapigadebe na kupinga kurubuniwa na nafasi za upendeleo zinazotumia kama kigezo kikuu cha kupeleka mwanamke kwenye uongozi iwe bungeni au halmashauri.

Aidha, AZAKI zinatakiwa zitoe elimu endelevu kwa wapigakura inayozingatia masuala ya haki za wanawake katika uongozi kitaifa kama sehemu muhimu ya kuendeleza demokrasia shirikishi, pia zionyeshe kwa vitendo imani thabiti isiyobagua wanawake na makundi mengine kwenye uchaguzi.

KING'ANG'ANIZI LUKASHENKO

# Baada ya kuishi ikulu miaka 30 bado anaamini pekee ana hati miliki urais

**Na Christina Mwakangale**

ALEXANDER Lukashenko (69), Rais wa Belarus, ametangaza tena nia ya kugombea urais katika uchaguzi unaofanyika mwakani 2025, linasema Shirika la Habari la Belarus, BeITA.

Rais huyo ameiongoza nchi hiyo kwa miaka 30 sasa, akinyakua madaraka tangu 1994, anatoa tamko hilo mbele ya wanahabari hivi karibuni, mara baada ya kupigakura za kuchagua wabunge na viongozi wa serikali za mitaa.

Anadai, hakuna anayeweza kutetea kiti chake kwa kuwa hakuna mtu, wala rais mwajibikaji kama yeye, anayeweza kuwaacha raia wake waliomuunga mkono wakati wa mapambano.

Lukashenko, ni rafiki mkubwa wa Rais wa Russia, Vladimir Putin, akiwa ameitawala Belarus tangu mwaka 1994, akimuunga mkono wakati huu wa vita vya Ukraine.

Licha ya kutangaza kutetea kiti hicho mwakani, anauona umbali uliopo kuifikia siku ya uchaguzi akisema: "Uchaguzi wa rais ni kipindi kirefu na mambo mengi yanaweza kubadilika."

Katika mahojiano na BBC Julai mwaka jana, anasema ikiwa kuna mtu anayeweza kusimulia hadithi mbaya zaidi, hakika ni kiongozi wa Belarus. Kadhalika, mwaka 2020, yalitokea maandamano nchini mwake kumpinga, yakielezwa na wachambuzi wa mambo kuwa, ni makubwa zaidi kuwahi kushuhudiwa katika historia ya nchi hiyo hivi karibuni.

Lukashenko, anayekabiliwa na upinzani mkali, ingawa mara kadhaa, anasema haondoki madarakani 'ng'o', licha ya kuwapo wimbi la maandamano kupinga utawala wake, Rais huyo wakati wa mahojiano na waandishi wa habari wa Russia, anasisitiza kuwa madai hayo si ya kweli na kwamba upinzani uliibiwa kura.



Rais wa Belarus, Alexander Lukashenko. **PICHA: REUTERS**

Upinzani nchini humo uliporwa ushindi mwaka 2020 katika uchaguzi mkuu, kwa mujibu wa DW. Watu wanaokadiriwa kufikia zaidi ya 100,000, walikusanyika katika uwanja wa uhuru wakiimba nyimbo na kubeba mabango ya kumshutumu Rais Lukashenko kama kiongozi muuaji na mnyanyasaji.

Hata hivyo, maandamano hayo hayakumtisha Lukashenko ambaye naye aliongoza mkutano wa wafuasi wake na kuwafananisha wapinzani wake kama panya.

### MPINZANI WAKE

Mgombea mkuu wa upinzani, Svetlana Tikhanovskaya aliyepambana na Lukashenko, wakati wa uchaguzi uliopita na kutangazwa mshindi wa uchaguzi huo mwaka 2020 kwa kupata asilimia 80, aliitisha maandamano hayo baada ya kukimbilia nchi jirani ya Lithuania, kwa mujibu wa DW.

Mwaka jana, pia kulikuwa na uvumi kuhusu afya ya Lukashenko, ingawa katika mazungumzo yaliyochukua karibu saa nne, alionekana imara, ianasema DW.

Marekani na Uingereza, hazimtambui kama rais halali wa Belarus na mwaka 2020, Wabelarus walimiminika mitaani kumshutumu kwa kuchakachua uchaguzi wa urais wa nchi hiyo. Maandamano hayo yalizimwa, BBC inasema. Anatuhumiwa na kesi ya mwanaharakati wa upinzani aliyefungwa jela Maria Kolesnikova, ikisema kwa miezi kadhaa, jamaa na mawakili wake wamekataliwa kumtembelea gerezani.

"Mara ya mwisho nilipokuhoji katika msimu wa vuli wa 2021, kulikuwa na wafungwa 873 wa kisiasa nchini Belarus," inamkumbusha Lukashenko.

Septemba mwaka 2021, Belarus ilimhukumu Maria Kolesnikova kwenda jela miaka 11 kwa hatia ya 'kula njama za kupindua rais.'

Mahakama ya Belarus, ilimhukumu mwanasiasa wa upinzani Kolesnikova, mmoja wa watu mashuhuri wa maandamano ya msimu wa joto wa 2020 kutumikia kifungo hicho.

Hukumu hiyo ilionyesha ukandamizaji dhidi ya upinzani kwa serikali ya Lukashenko na Umoja wa Ulaya uliilaani na kuikosoa kwa kuvunjwa haki za binadamu.

Maria Kolesnikova (39), alihukumiwa kwa kula njama kwa lengo la kuchukuwa madaraka, kuhamasisha vitendo vya kuhatarisha usalama wa taifa na kuundwa vuguvugu lenye msimamo mkali.

Viktor Babaryko, mpinzani mwingine na washtakiwa wenzake, wakili Maxime Znak, wamejikuta wanahukumiwa kifungo cha miaka 10. Kesi ya wapinzani hao wawili, ambao wamekaa gerezani kwa miezi 11, ilianza mapema Agosti 2021 na kufanyika katika kikao cha faragha.

Vyombo huru vya habari, mashirika ya kiraia na vyama vya upinzani pia vilikumbwa na ukandamizaji usiokoma kwa miezi. Mawakili wa upande wa utetezi pia walitakiwa kutozungumza juu ya yaliyomo kwenye kesi hiyo.

### UCHAGUZI WA BUNGE

Uchaguzi wa bunge na viongozi wa mitaa nchini Belarus, umefanyika mwishoni mwa mwezi uliopita, licha ya wito wa kuususia kutoka kwa upinzani, ukitarajiwa kuimarisha utawala wa Lukashenko, ambaye ameongoza taifa hilo kwa karibu miaka 30.

Lukashenko amedai kuwa mataifa ya magharibi yanajaribu kutumia kura hiyo, kuhujumu serikali yake, pamoja na kuyumbisha taifa hilo, lenye wakazi milioni 9.5. Wengi wa wagombea walioshiriki uchaguzi huo ni kutoka vyama vinne, vilivyosajiliwa vya Beyala Rus, Communist, Liberal na kile cha Labor na Justice.

Vyama vyote hivyo, vinaunga mkono sera za Lukashenko, wakati takribani vyama sita, vikiwa vimenyimwa usajili.

Kiongozi wa upinzani Sviatlana Tsihanouskaya, ambaye anaishi uhamishoni kwenye nchi jirani ya Lithuania, baada ya kugombea urais dhidi ya Lukashenko 2020, alitoa wito kwa wapigakura kususia uchaguzi huo. Uchaguzi huo ni wa kwanza tangu ule wa 2020 wenye utata na ambao ulitoa muhula wa sita kwa Lukashenko.

Wakati huo maandamano makali kote nchini humo, yalisababisha kukamatwa kwa zaidi ya watu 35,000, baadhi ya vyombo vya habari, vilipigwa marufuku, huku mashirika yasio ya kiserikali yakifungwa.

## Cheche za Makonda zilivyokula vichwa viongozi wasiowajibika

**INATOKA UK. 11**

Makonda akiwa Wilaya ya Pangani anachukizwa na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Isaya Mbenje, kushindwa kujenga zahanati kwa muda mrefu licha ya wananchi kuchanga fedha.

Halikadhalika mkoani Ruvuma anaagiza uongozi wa mkoa huo kushughulikia haraka malalamiko ya wakulima zaidi ya 1000, wanaodai kutapeliwa na mfanyabiashara, Christopher Njako, aliyechukua mahindi yao bila kuwalipa.

Wanadai Njako alinunua mazao yao bila kuwalipa na aliposhtakiwa aliachiwa kwa dhamana na kesi hiyo kukosa mwendelezo tangu 2021.

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo, Kanali Laban Thomas, aliomba kulishughulikia tatizo hilo huku Makonda akiwataka wananchi wajitokeze katika siku aliyoitaja ili changamoto yao ikatatuliwe. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbeya, Steven Katemba, hakubaki salama kwenye sekeseke la ziara ya Makonda.

Mabadiliko yamemhamishia Wilaya ya Sumbawanga mkoani Rukwa, mbele ya Makonda ziliibuliwa tuhuma mbalimbali ikiwamo watumishi wawili kudaiwa kuhamishwa kinyemela mkoani Mbeya kuficha ufisadi wa miradi.

Makonda akaongeza: "Nitakwenda kumweleza Waziri alete timu ya kuchunguza watu kwa kuwa hawana huruma wanakula hadi fedha za wagonjwa na kusababisha wananchi kukosa huduma."

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Elizabeth Nyema, akitakiwa kutoa majibu ya wapi zilipo Shilingi milioni 700, za vifaa tiba zilizotolewa kwa ajili ya kituo cha afya. Kitimoto kilikuwa pia kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nsimbo, Mohamed Ntandu, ambaye amehamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Magu.

Makonda anaumizwa na malalamiko ya Geoffrey Mboje, anayekutana naye jimboni Nsimbo mkoani Katavi, akieleza kunusurika kifo baada ya kupigwa mapanga 19 kwenye mgogoro wa ardhi.

"Nilikuwa natetea haki za wenzangu kwenye mgogoro wa ardhi. Jeshi la polisi halijawachukulia hatua wahusika hadi sasa." Anaeleza.

Katika mgogoro huo, Mkuu wa Wilaya ya Mpanda, Jamila Kimaro, baada ya kuwasikiliza Geoffrey Mboje na wenzake, alimpa kibali Mkurugenzi wa Nsimbo kuwaruhusu wananchi hao kuendelea na shughuli zao.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo, akatoa eneo hilo kwa watu wengine bila kumjulisha Mkuu wa Wilaya na kusababisha wananchi hao kuvamiwa na kuuliwa katika eneo hilo.

Makonda alimhoji Mkurugenzi Ntandu: "Kwa nini mpaka sasa hujaandika barua ya kujiuzulu wakati umesababisha mauti na maumivu kwa wananchi?"



## HABARI DODOMA

## Magereza kununua magari 28 ya kubeba wafungwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza linatarajia kununua magari 28 kwa ajili ya kupeleka na kusindikiza mahabusu mahakamani ili kuepusha tatizo la kuwachelewesha kusikiliza kesi zao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Mzee Ramadhan Nyamka, alisema kumekuwa na malalamiko mengi ya ucheleweshwaji wa mahabusu mahakamani, hivyo suala hilo linakwenda kutatuliwa.

"Tunakwenda kulimaliza tatizo hilo, hivyo hakutakuwa na ucheleweshwaji wa mahabusu tena kwenda mahakamani," alisema.

Alifafanua zaidi ya kuwa jeshi hilo linaendelea kujipanga kuhakikisha wanakamilisha masuala ya magari kwa ajili ya kuwapeleka mahabusu mahakamani.

Kamishna huyo alisema pia wapo katika harakati za kutafuta eneo la kujenga gereza hilo ili kulihamisha la Keko na kwamba ujenzi wa gereza moja ni takribani Sh. bilioni nane.

"Tuko katika harakati za kuhamisha gereza, tunasubiri tupate fedha kwa ajili ya kufanya ujenzi wa gereza hilo, pamoja na magereza mengine katika wilaya 46 ambazo hazina magereza," alisema Kamishna Jenerali.

Alisema eneo la Keko liko katikati ya wananchi, hivyo wanahitaji kulihamisha ili liwe pembezoni mwa mji, lakini liwe karibu na eneo la Mahakama.

Katika hatua nyingine, alisema Jeshi la Magereza limejipanga kuhakikisha linajitegemea kwa ulishaji vyakula kwenye magereza mbalimbali hapa nchini kama walivyoagizwa na serikali.

Alisema wanamagereza ambayo yapo kwa ajili ya kilimo, hivyo wataongeza kiwango cha kulima ili kufikia kiwango walichojipangia.

Alisema wanalima mazao mbalimbali, ikiwamo mpunga, mahindi, maharage na alizeti kwa ajili ya utoaji wa mafuta ya kupikia.

Alisema wameanza kujitegemea kwenye suala la chakula na hilo litakuwa ni kawaida, hivyo wamejipanga katika kuhakikisha wanafanya kilimo bora cha mazao mbalimbali.

Kadhalika, alisisitiza suala la matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kuepuka uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya magereza hapa nchini.

Alisema pia wamejipanga kuanza kutumia nishati mbadala ili kupunguza matumizi ya kuni kwa ajili ya kupikia chakula cha mahabusu katika magereza mbalimbali hapa nchini.

Alisema wataanza kutumia nishati mbadala kwa ajili ya kutumia katika magereza mbalimbali ili kupunguza uchafuzi wa mazingira nchini.

# 'Mifugo inayokula miti iliyopandwa ikamatwe, chinja, ifanywe kitoweo'

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya Manyoni mkoani Singida, Barnabas Mushi amepiga marufuku wafugaji kugeuza maeneo ya taasisi za serikali kuwa sehemu za malisho ya mifugo.

Aidha, ameagiza mifugo itakayokamatwa ikila miti iliyopandwa ikamatwe na kugawiwa kwa taasisi (shule) husika na wanafunzi wachinjiwe nyama ili kupoza machungu ya miti yao kuliwa.

Alisema hayo juzi wakati wa upandaji miti kuzunguka katika Shule ya Sekondari Sasilo iliyopo Tarafa ya Nkonko wilayani hapa kwa ajili ya kuhifadhi mazingira ya shule hiyo.

Katika zoezi hilo ambalo limefanywa na jumuiya hiyo jumla ya miti 3,780 imepandwa katika maeneo ya taasisi ya tarafa ya Nkonko kwenye kata za Nkonko, Iseke, Sanza, Sasilo, Heka na Chikola.

Mushi alisema ili kutunza miti inayopandwa isiharibiwe na mifugo aliwaomba watendaji wa vijiji na kata kukamata mifugo hiyo inayofanya uharibifu kwenye taasisi na kuigawa kwa taasisi husika.

"Niwaombe watendaji ukishika mbuzi imekula miti kama ni miti ya shule wape wanafunzi mbuzi huyo wamle wapunguze uchungu wa utunzaji na uhifadhi mazingira maana tukichekeana tutapoteza miti na tutakuwa na jangwa kisha tutaanza kuulizana kwanini atuna mvua," alisema.

Pia alisema moja ya majukumu ya jumuiya hiyo ni kusimamia afya, elimu, malezi, mazingirna utamaduni, hivyo ni jukumu la kila mwananchi kutunza mazingira.

Mwaka jana aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba akizindua upandaji miti katika wilaya zote za mkoa.

Pamoja na mambo mengine aliagiza wenyeviti wa halmashauri na madiwani kuhakikisha wanatunga sheria kali zitakazowafanya wafugaji kuwa makini na mifugo yao sambamba na kuweka faini kubwa kwa atakaye sababisha mfugo kula miti.

Aidha alitoa maelekezo kwa wakurugenzi wa halmashauri mkurugenzi kuhakikisha wananchi wanapunguza tabia ya ukataji miti ovyo na uchomaji wa mkaa.

Asilimia kubwa ya miti iliyopandwa wakati wa kampeni ya upandaji miti kandokando ya Barabara ya Manyoni-Singida imekufa kutokana na kuliwa na mifugo.



Makamu wa Rais, Philip Isdor Mpango, akizungumza kwenye banda la maonyesho lililofadhiliwa na mradi wa CookFund unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), wakati wa Kongamano la Wanawake la Nishati Safi ya Kupikia, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Wa pili kulia ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Doto Biteko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi TAMISEMI wapewa angalizo uchaguzi serikali mitaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imewaelekeza watumishi waliopewa jukumu la kusimamia maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu kuhakikisha yanafanyika kwa ufanisi na hayasababishi doa lolote kwa ofisi hiyo.

Maelekezo hayo yalitolewa jana jijini hapa na Naibu Waziri wa ofisi hiyo, Deogratius Ndejembi kwa niaba ya Waziri Mohamed Mchengerwa kwenye ufunguzi wa Baraza la Wafanyakazi la ofisi hiyo.

Alisema ofisi hiyo ni mratibu mkuu wa uchaguzi huo na maandalizi hayo yanahusisha uandaaji wa mpango kazi na bajeti ya uchaguzi huo, kuhakiki maeneo ya utawala yaliyopo na kuandaa rasimu ya kanuni za uchaguzi huo.

"Kufanya vikao na wadau wa ndani waratibu kwa upande wa halmashauri, wanasheria, makatibu tawala wa mikoa na wakuu wa wilaya, andaeni rasimu ya mwongozo wa utaoaji elimu ya mpigakura na kubainisha taratibu za ununuzi wa vifaa vya uchaguzi," alisema.

Alisema viongozi watakaochaguliwa ni sauti ya wananchi watachochea ustawi wa wananchi hivyo katika mchakato wa uchaguzi huo ushiriki wao ni muhimu sana.

"Watumishi walioteuliwa kuwajibika wawajibike ipasavyo ili kufanikisha uchaguzi huu...Wakati nakuja hapa Waziri Mchengerwa amewataka muweke kipaumbele katika kuandaa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa vizuri ili ofisi yetu isiingie doa lolote katika kusimamia uchaguzi huu," alisema.

Alibainisha kuwa ofisi hiyo inagusa maisha ya wananchi kila sekta, hivyo ni wajibu wa watumishi kuendelea kutekeleza matarajio na maono ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kutoa huduma bora zinazokidhi matarajio ya wananchi.

Aidha, alisema mabaraza ya wafanyakazi ni chombo cha kisheria kinacholenga kuongeza tija na uwajibikaji mahali pa kazi.

"Mabaraza ya wafanyakazi yatumike kujadili malengo na mipango ya taasisi ikiwamo maslahi ya watumishi, mnatakiwa kujadili utendaji kazi wenu wa kila siku," alisema.

Hata hivyo, alihimiza usimamizi wa mipango ya bajeti ili kufikisha huduma bora kwa wananchi.

Kadhalika, alisema serikali itaendelea kutatua kero zilizopo ikiwamo uhaba wa wafanyakazi.

Naye Kaimu Katibu Mkuu, Dk.Charles Msonde alisema kikao hicho cha baraza pamoja na mambo mengine kitajadili na kupitisha bajeti ya ofisi hiyo kwa mwaka 2024/25.

Naibu Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Dk.Wilson Mahera aliahidi watumishi wa ofisi hiyo watatekeleza ipasavyo maelekezo yaliyotolewa na serikali.





# Taarifa ya mapato na matumizi yaiponza kamati ya shule

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

DIWANI wa Kata ya Kijombe Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe, Seylvester Kigola, ameagiza kuvunjwa kwa kamati ya Shule ya Msingi Ikwavila kutokana na kulalamikiwa na wazazi kwa kutosoma taarifa ya mapato na matumizi, kushindwa kusimamia mali za shule.

Akizungumza katika kikao cha shule, Kigola alisema kutokana na malalamiko hayo hakuna haja ya kuendelea kuwa na kamati hiyo kwani wazazi hawatakuwa na mwamko wa kuendelea kutoa michango.

"Nikisema hili donda niliache ni changamoto sasa naomba nitoe maelekezo, naamini wazi nikisema niiache kamati hii ya shule iendelee wazazi hawatachanga michango hapa, wengine wataaminisha watoto au kufanya figisu kwa walimu wetu kupitia kamati ya shule," alisema Kigola.

Diwani Kigola aliwataka wazazi kuchagua kamati ya chakula ambayo itasimamia utaratibu wa watoto kupata chakula shuleni na kulinda mazao yanayotolewa kwa ajili ya chakula.

"Ni kosa kubwa kuweka malezi ovyo kwa watoto wetu, si vizuri sana kuona watoto wanazurura usiku niwaombe wazazi acheni tabia ya kuwaruhusu watoto kukaa kwenye kumbi za kuonyeshea mpira usiku," alisema Kigola.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya shule hiyo, Joseph Ng'amilo, alisema ameridhishwa na maamuzi ambayo yametolewa na diwani huyo na kueleza kuwa malalamiko hayo yamesababishwa na wajumbe wa kamati hiyo kumwachia majukumu pekee yake.

"Nimeridhika kabisa sina kinyongo chochote ni usimamizi tu kwa sababu shida uliyokuwapo ni kama kamati ya shule haikuwa vizuri kwenye suala la usimamizi kwa sababu asilimia kubwa kama nilikuwa mwenyewe," alisema Ng'amilo.

Mwenyekiti Kijiji cha Ikwavila, Samweli Mdapo, alisema atahakikisha uchaguzi wa kuchagua kamati mpya ya shule unafanyika kwa wakati ili kukuza taaluma ya shule hiyo.

Nao baadhi ya wazazi katika Kijiji cha Ikwavila, Neema Mfanyakalendi, Faraja Mubanga, Histi Kig'wenyu na Thobias Chavala walisema changamoto kubwa ni kamati hiyo kushindwa kusimamia vyema shule hiyo.



Ofisa Rasilimaliwatu wa Mgodi wa Sotta, Gloria Kasanga, akizungumza na wanawake wakazi wa Kata ya Igalula na wafanyakazi wa mgodi huo, katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, wilayani Sengerema, mkoani Mwanza, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wauza samaki, maofisa serikali waingia katika mgogoro

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MGOGORO umeibuka baina ya wajasiriamali wanaouza samaki katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya na maofisa wa serikali waliokuwa wanaendesha operesheni ya kuwakamata wajasiriamali hao, kwa madai ya kufanya biashara hiyo bila kuwa na vibali.

Maofisa hao wanaodaiwa kutoka katika Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kitengo cha kilimo, mifugo na uvuvi wanadaiwa kuvamia maeneo ya wajasiriamali hao usiku, kupora samaki na kuzifungia ofisini hali ambayo inawasababishia hasara.

Hivi karibuni wajasiriamali hao waliiomba serikali kuwasaidia kuwaondoa maofisa hao wakidai kuwa operesheni wanazozifanya siyo halali kutokana na maofisa hao kuingia mitaani na kuanza kuwakamata muda ambao siyo wa kazi na kwamba hawana elimu yoyote kuhusiana na vibali vinavyotakiwa.

Happy Mwaipungu alisema maofisa hao walipohifadhi samaki zao ofisini waliwataka kulipa Sh. 20,000 ili wawarejeshee bidhaa hizo, huku pia wakilazimishwa kujiunga kwenye chama cha wafanyabiashara wa samaki kwa gharama ya Sh. 200,000.

Alisema mtaji wake ni Sh. 5,000 na hivyo hana uwezo wa kulipa gharama zinazohitajika na hivyo akaiomba serikali iwasaidie ili waweze kufanya biashara yao kwa uhuru.

"Sisi hapa asilimia kubwa mitaji yetu ni chini ya Sh. 10,000 kwa hiyo hatuna uwezo wa kulipa Sh. 20,000, tunapata faida kidogo sana kwenye biashara hii kwa ajili ya kutusaidia kuendesha maisha na watoto wetu," alisema Happy.

Esther Jackson alisema maofisa hao baada ya kuwapora samaki zao hawakuhifadhi kwenye ofisi ya serikali na badala yake wakahifadhi kwenye ofisi ya chama cha wafanyabiashara wa samaki wanaouzia ndani ya Soko la Tarafani.

Alisema wao wanauza nje ya soko ambako wanalipa ushuru na mapato mengine ya serikali na kwamba hawauzi muda wote na badala yake wanauza kuanzia jioni muda ambao walikubaliana na wafanyabiashara wa ndani ya soko ili kutoingiliana.

Alisema baadhi ya samaki waliochukuliwa walikuwa wamehifadhiwa kwenye ndoo hali ambayo itasababisha samaki hao kuharibika na kuwaingiza hasara.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara wadogo maarufu kwa jina la machinga Kata ya Utengule Usongwe, Calvin Lunda alisema baada ya maofisa hao kukamata bidhaa za wajasiriamali waliamua kuwahoji lakini hawakuwapa ushirikiano.

Alisema waliamua kuwasiliana na Ofisa Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Gideon Mapunda, ambaye alisema hajawatuma wakafanye kazi hiyo jambo ambalo liliwapa wasiwasi.

Alisema muda ambao maofisa hao waliingia ulikuwa ni muda ambao sio wa kazi kwa maofisa wa serikali na hivyo wakahisi kwamba pengine walikuwa ni wahuni.

Gideon ambaye ni Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alikiri kutokea kwa mgogoro huo na kwamba kilichosababisha ni wajasiriamali hao kutokuwa na uelewa wa taratibu za kuuza samaki.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya uvuvi, mtu yeyote anayefanya biashara ya mazao ya uvuvi ni lazima awe na vibali na kwamba Sh. 20,000 ambazo wajasiriamali hao walikuwa wanatozwa ni kwa ajili ya kuwakatia leseni.

Alisema leseni za biashara ya mazao ya samaki zinatofautiana kulingana na ukubwa wa biashara kwa maelezo kuwa bei hizo zinaanzia Sh. 20,000 na kuendelea.

# DC awatangazia kiama w'biashara wanaouza sukari bei juu

**Na Elizabeth John,** MAKETE

SERIKALI wilayani Makete mkoani Njombe, imetangaza kuanza kuwachukulia hatua za kisheria wafanyabiashara wanaouza sukari kwa bei ya juu tofauti na bei elekezi iliyotolewa na serikali.

Mkuu wa wilaya hiyo, Juma Sweda alitoa tahadhari hiyo wakati wa mkutano wa hadhara na wakazi wa Kata ya Bulongwa wilayani hapa, uliokuwa na lengo la kusikiliza kero.

Alitoa agizo hilo baada ya wananchi wa kata hiyo kulalamikia kupanda kwa gharama kubwa ya ununuzi wa sukari ambayo imekuwa ikiuzwa kati ya Sh. 5,000 hadi Sh. 6,000 kwa kilo moja.

"Katika Wilaya ya Makete bei ya kuuzia sukari ni kuanzia Sh. 2,700 hadi Sh. 3,000, wafanyabiashara wote niwatake kufuata hiyo bei na atakayekiuka muda siyo mrefu mtapata majibu ya mnachokifanya kwa sababu haiwezekani sukari inauzwa Sh. 5,000 hadi Sh. 6,000 wakati miongozo ya bei elekezi ipo na mnatakiwa kuitumia," alisema Sweda.

Hata hivyo Sweda aliwataka wakazi wa Kata ya Bulongwa, kutoendekeza migogoro isiyokuwa na tija ambayo imekuwa ikipelekea sintofahamu ya umiliki wa ardhi kwenye baadhi ya maeneo ya miradi na kuchelewesha maendeleo ndani ya kata.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Makete, Dk. Ligobert Kalisa, aliwataka wananchi wilayani hapa kuwa na bima ya afya iliyoboreshwa ili wawe na uhakika wa kutibiwa pale wanapopata changamoto za kiafya.

Kwa upande wa baadhi ya wananchi wakizungumza kwenye mkutano huo walisema bado wafanyabiashara wanauza sukari kwa bei wanazotaka wao.

Walisema licha ya matamko mbalimbali ambayo yanatolewa na serikali lakini kwao hakuna unafuu.

"Kwa kweli tulikuwa tunaumia sana sukari ilifika hadi kilo moja Sh. 6,000, ukizingatia unafamilia kubwa maisha nayo magumu fedha inapatikana kwa tabu kwa hiyo tunaiomba sana serikali itusaidie," alisema Jovita Sanga.

Naye mfanyabiashara John Tweve alisema wanaopandisha bei ya sukari siyo wao bali ni wafanyabiashara wakubwa hali inayosababisha na wao kuuza bei ambayo itawapa faida.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alifanya ziara kwa wafanyabiashara na aliahidi kuendelea kusimamia bei elekezi ya sukari na kuwataka wafanyabiashara kutouza sukari zaidi ya Sh. 3,200 kwenye mkoa huo na kwamba hatua za kisheria zitachukuliwa kwa watakaokiuka agizo hilo.



## Mwakilishi Kwahani ataja mafanikio ya serikali sekta ya elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Jimbo la Kwahani, Yahya Rashid Mamba amesema Serikali inaimarisha miundombinu ya elimu kwa kujenga majengo ya kisasa, kuboresha vifaa vya kufundishia na kuongeza idadi ya walimu shuleni.

Aliyasema hayo jana katika Shule ya Msingi Sebleni iliyopo Unguja wakati wa hafla ya kuwapongeza na kuwazawadia wanafunzi waliofanya vizuri katika mitihani yao, ambapo wamekabidhiwa zawadi mbalimbali ikiwemo fedha na vifaa vya shule.

Alisema uwekezaji unaofanywa na Serikali katika kuimarisha elimu ni lazima uendane sambamba na uwekezaji wa masomo ya sayansi, ili kutengeneza vijana watakaoweza kuisaidia nchi yao.

Aidha alisema kutokana na hali ya dunia kuipa kipaumbele teknolojia kuna haja ya kuimarisha mifumo ya sayansi katika elimu ili kurahisisha upatikanaji wa huduma katika jamii.

Hata hivyo aliwataka walimu wa shule hiyo kufundisha kwa bidii ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Bimkubwa Mbwana Kombo, alisema wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwemo mashine ya kurudufisha, tangi la kuhifadhia maji na uhaba wa vyoo ikilinganisha na idadi kubwa ya wanafunzi wanaosoma katika shule hiyo.

Alisema ufaulu wa shule hiyo umechangia kwa kiasi kikubwa ushirikiano uliopo baina ya Serikali, walimu, wazazi na wanafunzi wenyewe.

**Hata hivyo aliwataka walimu wa shule hiyo kufundisha kwa bidii ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.**

# Walimu vyuoni waagizwa kuhamasisha wanafunzi kutumia sensa katika utafiti

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WALIMU wa vyuo vikuu wametakiwa kuwahamasisha wanafunzi kutumia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, kwa ajili ya kufanya utafiti mbalimbali ili kuisaidia serikali kupanga mipango yake ya maendeleo.

Agizo hilo limetolewa na Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Balozi Muhammed Haji Hamza visiwani Zanzibar wakati wa kikao cha usambazaji wa matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa makundi maalum.

Alisema kundi la vyuo vikuu lina umuhimu mkubwa katika kufanikisha usambazaji wa matokeo ya sensa kutokana kutumia taarifa wakati wanapofanya utafiti wao.

Hivyo alisema walimu wanawajibu wa kuyatumia matokeo hayo kwa ajili ya kufundishia vyuoni ili wanafunzi wapate kuelewa namna ya kutumia takwimu kwa usahihi.

Alisema matokeo ya sensa yanaonyesha mambo mbalimbali katika sekta ya elimu, hivyo iwapo yatatumika vizuri yatawasaidia wanafunzi ambao wanahitaji kufanya utafiti wa viashiria vya kielimu kwa ajili ya kutambua maendeleo ya elimu tangu mwaka 1964 na kuishauri serikali katika kupanga mipango yake ya maendeleo kwa wananchi.

Balozi Hamza akizungumzia lengo la serikali kusambaza matokeo ya sensa kwa makundi mbalimbali alisema ni pamoja na jamii kupata uelewa wa namna serikali inavyopanga mipango yake ya maendeleo, ikiwemo utekelezaji wa miradi mbalimbali, kufanya maamuzi sahihi ambayo yatatolewa kwa ushahidi wa takwimu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Takwimu, Balozi Amina Salum Ali, alisema iwapo walimu watayatumia matokeo hayo watapata nyenzo ya kufundishia na kujenga hoja kwa wanafunzi.

Alisema nchi mbalimbali duniani zinategemea zaidi kutumia takwimu sahihi kwa ajili ya kupanga mipango yake, hivyo kupitia matokeo hayo ya sensa yataisaidia nchi kuwa na takwimu sahihi za watu kupanga mipango yake kwa urahisi.

Akitoa mada kuhusu umuhimu wa baadhi ya viashiria vya kiuchumi, kijamii na mazingira vinavyotokana na Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 iliowasilishwa na Abdulmajid Ramadhan Jecha kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, alisema kiwango cha watu wanaojua kusoma na kuandika Zanzibr kimeongezeka kutoka asilimia 84.2 mwaka 2012 hadi asilimia 90.6 mwaka 2022.

Alisema zaidi ya asilimia 77 watu wenye umri wa miaka 15 na kuendelea kutoka mikoa yote ya Zanzibar wanajua kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili na Kingereza na lugha nyingine.

Aidha alisema kuwa Mkoa wa Mjini unakiwango kikubwa cha watu wanaojua kusoma na kuandika, ambapo Mkoa wa Kaskazini Pemba unakiwango kidogo cha watu wanaojua kusoma na kuandika.

Meneja wa Viwango Uratibu na Utafiti, Hamisa Suleiman Faki, alisema taasisi ama wageni ambao wanahitaji kufanya utafiti mbalimbali Zanzibar wanapaswa kuwa na vibali kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.




Mbunge wa Jimbo la Segerea, Bonnah Kamoli (wa pili kushoto), akimkabidhi mmoja wa madaktari (kulia), msaada wa vifaa vya kujifungulia kinamama katika Zahanati ya Bonyokwa mwishoni mwa wiki, msaada walioutoa kwa kushirikiana na Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Katikati (mwenye nguo nyekundu) ni Mwenyekiti wa jukwaa hilo, Rehema Sanga. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# Serikali yaipa kongole Taasisi ya Mwanamke Initiative

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imesifu juhudi zinazochukuliwa na taasisi ya Mwanamke Initiative Foundation katika kutoa kipaumbele maendeleo ya sekta ya elimu katika Mkoa wa Kusini Unguja.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari, Asya Iddi Issa, katika hafla ya kuwapongeza wanafunzi waliofanya vizuri katika mitihani ya kidato cha nne katika Shule ya Hasnuu Makame Kusini Unguja.

Alisema taasisi hiyo inamchango mkubwa ikiwemo kufuatilia na kusimamia maendeleo ya elimu katika Mkoa wa Kusini Unguja, huku wakilenga katika ufaulu wa kidato cha nne.

Alisema wizara imefarajika kuona matokeo mazuri ya ufaulu kwa wanafunzi katika shule za Mkoa wa Kusini Unguja katika mtihani wa taifa.

Aidha aliwataka wazazi kufuatilia maendeleo ya watoto wao, kuhakikisha wanapata ufaulu mzuri wa mitihani ya taifa kwa kushirikiana na walimu.

Mwenyekiti wa taasisi ya Mwanamke Initiative Foundation, Wanu Hafidh Ameir, alisema uongozi wa shule hiyo umekuwa ukifanya kazi pamoja na taasisi yake katika kuunga mkono maendeleo ya sekta ya elimu.

Aidha aliwapongeza walimu na wanafunzi wa shule hiyo kwa kupata matokeo mazuri katika mitihani ya taifa kidato cha nne.

Alizitaja juhudi zilizochukuliwa na uongozi wa taasisi yake ni pamoja na kupeleka walimu 70 kwa ajili ya kuongeza nguvu katika ufundishaji wa masomo ya sayansi.

Aidha alisema juhudi hizo zinakwenda sambamba na ushirikiano wa wadau wa taasisi za elimu kuona malengo yanafikiwa.

"Taasisi ya Mwanamke Initiative imejipanga kikamilifu kuona maendeleo ya sekta ya elimu katika Mkoa wa Kusini Unguja yanafikiwa na kupata mafanikio makubwa katika ufaulu wa wanafunzi wa sekondari" alisema.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Sekondari ya Hasnuu Makame, Issa Ali Haji Ali, alisema mafanikio ya ufaulu wa wanafunzi yanatokana na Ushirikiano ikiwemo ya wazazi pamoja na taasisi hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikifuatilia maendeleo ya elimu katika Mkoa wa Kuisni Unguja.

Akisoma risala ya wanafunzi, Naimani Mussa alisema tathmini inaaonesha ufaulu umeongezeka kwa asilimia 80 kutoka 40 ya miaka miwili iliyopita.

Katika hafla hiyo taasisi hiyo ilitoa magodoro 52 kwa ajili ya wanafunzi wa shule hiyo, huku Rais Samia Suluhu Hassan akitoa Sh.500,000 kwa kila mwalimu pamoja na Sh.500,000 kwa wanafunzi waliofanya vizuri.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
CHANGE OF NAME BY DEED POLL
(Registration of Documents Act (Cap 117) R.E 2002)

By this deed, I the undersigned, **THERESIA STEPHEN MBIPA** of Postal Office Box No. 90053 DAR ES SALAAM do hereby absolutely renounce and abandon the use of my said former names of **TEREZYA S. MBIPA, THERESIA M. STEPHEN, TEREZYA MBIPA, THEREZIA STEPHEN MBIPA,** and **THEREZIA STEPHEN NHWAGI** and in lieu thereof do assume as from the date hereof the name **THERESIA STEPHEN MBIPA** and in pursuance of such change of name as aforesaid I hereby declare that I will at all times hereafter in all records deeds and instruments in writing and in all actions and proceedings and transaction and upon all occasions whatsoever use and sign the said name of **THERESIA STEPHEN MBIPA** as my name in lieu of my said former names of **TEREZYA S. MBIPA, THERESIA M. STEPHEN, TEREZYA MBIPA, THEREZIA STEPHEN MBIPA** and **THEREZIA STEPHEN NGWAGI** renounced as aforesaid.
And I hereby authorize and request all persons to designate, describe and address me such assumed name of **THERESIA STEPHEN MBIPA** only.
In witness whereof I have hereunto set my hand this 29th day of February, 2024.

SIGNED and DELIVERED by the said THERESIA STEPHEN MBIPA who is Known to me personally/identified to Me by ______ the latter being Known to me personally at Dar es Salaam this 29th day of February 2024

Before me:
Name: Rita Dawson Chitemna
Designation: ADV/Comm. for oaths
Signature:



## KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**PATRICK JAMES MNAHELA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 972 DNT** CHASSIS NO: **SSTKE7T000001311,** ENGINE NO ***162FMJSST01311*** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA: **ARU/ARU/RB/58300/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JONA KULWA JOSEPH** Wa Nyahanga Mjini Kahama, anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 474 DJQ** aina ya SCANIA. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi.
**KAH/RB/123/2024.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**KIV COMPANY LTD**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 154 ANM Toyota Land Cruiser .** Chasses Namba **0003602,** Engine Namba **0008590** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Polisi Taarifa :
**KIL/ MOS/RB/480042/2021**

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA

**Probate and administration Cause No 4828 of 2024**
**In the matter of the estate of the late VENANCIA FREDDY MTEWELE**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by MAXIMILIAN FREDY MTEWELE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 25 day of 3...................... 2024
Dated at Dodoma this 12 day of 3................2024

PRINCIPLE/RESIDENT MAGISTRATE

Summons to appear (O. VR. 20 (1) of (CPC)
(Substituted Service)

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(LAND DIVISION) AT DAR ES SALAAM

MISC.LAND APPLICATION NO. 747 OF 2023

JEHANGIR AZIZ ABDULRASUL..............APPLICANT

VERSUS

MS BENANDYS LTD & ANOTHER............RESPONDENT

TO: (1) MS BENANDYS LIMITED (2) JOSHUA E. MWAITUKA t/a RHINO AUCTION MART

NOTICE OF DATE OF HEARING

**WHEREAS:** The above named APPLICANT has institute the CASE against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized Agent or 18TH day of MARCH, 2024 at 09:00AM Before Hon A. MSAFIRI, JUDGE in the morning to answer the said CASE and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your REPLY.
**TAKEN NOTICE** that, in default of your appearance on that day the said matter will be heard and determined in your absence.
Given under my hand and the seal of this Court, this 08TH day of MARCH, 2024.

DEPUTY REGISTRAR

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA

**Probate and administration Cause No 5159 of 2024**

**In the matter of the estate of the late JAMES NOEL WISALE of Makulu within Dodoma City**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by JUMAA MLINGI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 21 day of 3...................... 2024
Dated at Dodoma this 12 day of 3................2024

RESIDENT MAGISTRATE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO
YA WILAYA YA MOROGORO

KITUO CHA CHAMWINO MKOA WA MOROGORO

Usimamizi wa Mirathi Na...9/2024

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU: MOHAMED SAID MOHAMED wa MOROGORO

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA JUMANNE MOHAMED MAZOLA

TANGAZO
(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 17 Mwezi 4 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 11 mwezi 3 mwaka 2024

HAKIMU

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA

Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA

Shauri la madai/Ndoa Na. 22/2024

Jina la Mdai ..............................SOFIA KEYA NYANGAI

Jina la Mdaiwa ............................YUSUPH ADAM SUDI

KUITWA SHAURINI MDAIWA

(Kanuni ya (18) ya Kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)

**KWA: YUSUPH ADAM SUDI**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TALAKA MGAWANYO WA MALI**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 20 mwezi 03 mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinanyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii Imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 11 Mwezi 03 Mwaka 2024.

IN THE DISTRICT COURT OF KYELA
KYELA

PROBATE APPEAL CASE NO 2925 OF 2024

ALFRED MWANDALI..................APPELLANT

VERSUS

ULIMBOKA GREEN...............RESPONDENT

TO
ULIMBOKA GREEN,

**TAKE NOTICE** that the above mentioned case has been set down for Hearing on 14th day of March 2024 at 08:30 a.m in forenoon or thereafter at the District Court.

You must produce on that day all the witnesses upon whose evidence and all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

Given under my hand and the seal of this court this 8th day of March 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE I/C
KYELA

## TANGAZO LA MNADA

Held, Cops, NALC Marmboto and EIE Auctioneer Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Magari Jijini Dar es salaam na Arusha Mteja anashauriwa kulipa deni ndani ya siku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | DHAMANA | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Salimu Issa Juma | Toyota Crown T136EEJ Ipo Dar es salaam | 27.03.2024 |
| Jimmy Eliud Mchao | Mitsubishi Aitreck T926DHH Ipo Dar es salaam | 27.03.2024 |
| Salim Yarabi Ally | Honda crossroad -T177EBX Ipo Dodoma | 27.03.2024 |
| Michael Hugo Pius | Toyota Passo T822DCJ Ipo Dar es salaam | 27.03.2024 |
| Mary Zakaria Lyapa | Nissan Civilian T427DLY Ipo Dar es salaam | 27.03.2024 |

**Masharti ya Mnada.**
1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa Mawasiliano Piga**
**0677014355 (Fanikiwa)**

KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA

MASJALA NDOGO YA TEMEKE
(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)

MIRATHI NA 4259 YA MWAKA 2024.

MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU

ROSEMARY MABEL KIGADYE

NA

VICTOR LYSON MWAKIMI..................MWOMBAJI

TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 25 Mwezi Machi, 2024, Saa 5:00 Asubuhi. Siku ambayo Shauri hili limepangwa kusikilizwa mbele ya Mhe. Jaji S.S. Sarwatt.
Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 5 Mwezi wa Machi, 2024.

NAIBU MSAJILI


## OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
website: www.ippmedia.com

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.


Kwa

HABARI KIMATAIFA

# Marekani yawawekea vikwazo wanaowafadhili al-Shabaab

**WASHINGTON,** Marekani

OFISI ya Wizara ya Fedha ya Marekani inayohusika na Udhibiti wa Mali za Kigeni (OFAC), imeyawekea vikwazo mashirika 16 na watu binafsi, ambao inasema wanahusika katika mtandao mpana wa biashara unaozunguka Pembe ya Afrika, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Cyprus.

Ilisema jana kuwa mtandao huo huchangisha na kutakatisha fedha, za kufadhili shughuli za wanamgambo wa al-Shabaab, kundi la kigaidi lenye mafungamano na al-Qa'ida.

Ofisi hiyo inasema watu binafsi ndani ya mtandao huo ni pamoja na wafanyabiashara wenye ushawishi mkubwa katika eneo hilo ambao hutoa msaada wa kifedha kwa al-Shabaab, kikundi kilichohusika na baadhi ya mashambulizi mabaya zaidi ya kigaidi katika historia ya Afrika Mashariki.

Makampuni hayo ni pamoja na Crown Bus Service ya Kenya, Haleel Comodities LLC na Qemat Al Najah General Trading. Wafanyabiashara waliolengwa ni pamoja na Faysa Yusufu Dini anayeishi nchini Kenya, Hassan Farah Mohamed na Mohamed Jumale Ali Awale.

"Mashambulizi haya yamesababisha vifo vya maelfu ya raia wasio na hatia. Watu hawa wanawekewa vikwazo kwa mujibu wa Agizo la Utendaji (E.O.) 13224, kama linalo makundi ya kigaidi na viwezeshaji vyao," ilisema taarifa ya wizara hiyo.

"Marekani imejitolea kufanya kazi na washirika wa kikanda ili kung'oa mitandao ya ufadhili wa ugaidi na mashirika wanayotumia vibaya, kutafuta na kuhamisha fedha," alisema naibu wa waziri wa wizara ya fedha, anayehusika na masuala ya ugaidi na ujasusi wa fedha, Brian Nelson (pichani chini).

"Hatua ya 'leo' jana ni sehemu ya juhudi nyingi za Wizara ya Fedha kuunga mkono juhudi za serikali ya Somalia dhidi ya al-Shabaab moja ya nguzo tatu katika kampeni yao ya kudhalilisha kundi hili baya la kigaidi," alisema. **VOA**



# Kagame uso kwa uso na Rais Felix Tshisekedi

**KIGALI,** Rwanda

RAIS wa Rwanda, Paul Kagame, amekubali kukutana na mwenzake wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Felix Tshisekedi, ili kujadili hali ya usalama katika eneo lenye hali tete la Mashariki mwa Kongo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Waziri wa Mambo ya Nje wa Angola, Tete Antonio alisema imeamuliwa kuwa Rais Kagame atakutana na Rais Tshisekedi kwa tarehe itakayopangwa na mpatanishi.

Tamko hilo lilifuatia mkutano katika mji mkuu wa Angola Luanda baina ya wawili hao na Rais wa Angola Joao Lourenco ambaye ni mpatanishi wa Umoja wa Afrika (AU). Ikibainishwa kuwa ofisi ya Rais wa Rwanda imeonesha nia ya kushiriki upatikaji wa amani mashariki ya Kongo.

**Rais Tshisekedi anadai kuondolewa kwa wanajeshi wa Rwanda kutoka katika ardhi ya Kongo, kusitishwa kwa mapigano na uasi wa M23 kabla ya kukutana na Rais Kagame.**

Katika ukurasa wa X, zamani Twitter ofisi ya rais wa Rwanda iliandika kwamba wakuu wa nchi wamekubaliana juu ya hatua muhimu za kushughulikia sababu za mzozo, na kudumisha haja ya mchakato wa Luanda na Nairobi ili kufikia amani na utulivu katika eneo hilo.

Mwishoni mwa Februari, ofisi ya rais wa Kongo ilisema kwenye ukurasa wake wa X, kwamba Rais Tshisekedi kimsingi ameonesha utayari wa kukutana na mwenzake wa Rwanda.

"Rais Tshisekedi anadai kuondolewa kwa wanajeshi wa Rwanda kutoka katika ardhi ya Kongo, kusitishwa kwa mapigano na uasi wa M23 kabla ya kukutana na Rais Kagame," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.


Aidha, ilielezwa kuwa Kagame na Tshisekedi walikutana mara ya mwisho katika mji mkuu wa Ethiopia, Addis Ababa Februari 16 kando ya mkutano wa viongozi wa AU, wakati wa mkutano mdogo wa kilele ulioandaliwa na Lourenco.

Kwa mujibu wa vyanzo viwili vya kidiplomasia vya Addis Ababa, mkutano huo ulikuwa wa mvutano mkubwa na ulimalizika kwa kurushiana maneno makali.

Kwa mujibu wa UN mapigano kati ya waasi wa M23 na vikosi vya Kongo yamepamba moto mashariki mwa DRC, na kuwafanya zaidi ya watu 100,000 kuyahama makazi yao. Huku taifa hilo, UN na mataifa ya Magharibi yakiishutumu Rwanda kwa kuunga mkono M23, madai ambayo serikali ya Kigali inayakanusha.

Baada ya miaka minane ya utulivu, waasi wa M23 walichukua tena silaha mwishoni mwa 2021 na kuyateka maeneo makubwa ya eneo la Kivu Kaskazini, ambalo linapakana na Rwanda.

Pia mwishoni mwa mwaka 2023 UN ulikadiria kuwa karibu watu milioni saba walikimbia makazi yao nchini Kongo, wakiwamo milioni 2.5 katika eneo la Kivu Kaskazini pekee. **DW**



Rais wa Rwanda, Paul Kagame, Rais wa Angola Joao Lourenco na Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Felix Tshisekedi walipokuwa mjini Luanda, Angola Julai 6, 2022. **PICHA: MTANDAO**

# Waziri mkuu wa Haiti ajiuzulu

**PORT-AU-PRINCE,** Haiti

MWENYEKITI wa kundi la nchi za Caribbean amesema Waziri Mkuu wa Haiti, Ariel Henry amejiuzulu, kutokana na kuongezeka kwa shinikizo la kumtaka aachie ngazi na ghasia zinazoendelea nchini humo.

Ilielezwa kuwa hatua hiyo inakuja baada ya viongozi wa kanda kukutana nchini Jamaica kujadili mpito wa kisiasa nchini Haiti. Ikibainishwa kuwa kwa sasa Henry yuko Puerto Rico baada ya kuzuiwa na magenge yenye silaha kurudi nyumbani, baada ya kuongoza nchi hiyo tangu kuuawa kwa aliyekuwa kiongozi wa nchi hiyo, Rais Jovenel Moïse Julai 2021.

Akizungumza jana mjini Kingston, mwenyekiti wa Jumuiya ya Caribbean na Rais wa Guyana Irfaan Ali, alisema wanatambua kujiuzulu kwake baada ya kuanzishwa kwa baraza la mpito la rais na kumtaja waziri mkuu wa muda.

Magenge yenye silaha kali yamedhibiti mitaa ya mji mkuu wa Haiti wa Port-au-Prince katika siku za hivi karibuni, yakitaka waziri mkuu huyo ambaye hajachaguliwa ajiuzulu.

Henry alikuwa nchini Kenya kutia saini mkataba wa kutumwa kwa kikosi cha usalama cha kimataifa kusaidia kukabiliana na ghasia wakati muungano wa magenge uliposhambulia vituo vya polisi na kuvamia magereza mawili makubwa zaidi nchini Haiti.

Ndege iliyokuwa imembeba Henry ilizuiwa kutua kutokana na msururu wa mashambulizi katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Haiti.

Marekani iliyokuwa kwenye mazungumzo mjini Kingston ilisema waziri huyo alieleza nia ya kurejea Haiti lakini hali ya usalama inahitaji kuimarishwa kabla hajaweza kufanya hivyo.

Ofisa mkuu wa Marekani, alisema Henry alifikia uamuzi wa kujiuzulu Ijumaa wiki iliyopita lakini alikuwa akisubiri tangazo rasmi ili mazungumzo yafanyike.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Blinken alitoa dola milioni 100 (Sh. bilioni 254.5) kwa kikosi cha usalama kinachoungwa mkono na Umoja wa Mataifa (UN) chenye askari 1,000 ambacho Kenya inatarajiwa kuongoza nchini Haiti.

Inaelezwa kuwa Baraza la Jumuiya ya Caribbean limepewa mamlaka ya haraka kumteua waziri mkuu wa muda, ikielezwa kuwa yeyote anayenuia kugombea katika uchaguzi ujao wa Haiti hataweza kushiriki. **BBC**

# TFF SASA YASUBIRI MAJIBU CAF UKAGUZI VIWANJA VYA CHAN

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu (TFF), limesema linasubiri majibu kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF), baada ya kumaliza ukaguzi wa viwanja vitakavyotumika kwenye Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zinazotarajia kufanyika hapa nchini kwa ushirikiano wa Kenya na Uganda, Septemba mwaka huu.

Wakaguzi kutoka CAF, juzi Machi 11 walifanya ziara kwenye viwanja vya mazoezi vitakavyotumiwa na timu zitakazokuja hapa nchini kushiriki mashindano ya CHAN, ambapo kwa upande wa Tanzania mechi hizo zitachezwa Dar es Salaam pamoja na visiwani Zanzibar.

Mkurugenzi wa Idara ya Masoko, Sheria na Habari wa TFF, Boniface Wambura, amesema timu ya wakaguzi kutoka CAF imemaliza kazi yake na wameahidi baada ya siku 14 watatuma ripoti ya matokeo ya ukaguzi wao.

"Ni kweli kwamba tulikuwa na ugeni wa ukaguzi wa viwanja kwa ajili ya fainali za CHAN mwaka huu na tulikuwa na timu ya watu kutoka CAF, walianzia ukaguzi Uganda, wakaenda Kenya na wamekuja kumalizia Tanzania, lakini wametuambia kuwa huu ni ukaguzi wa awali kuona miundombinu, kikubwa walikuwa wanaangalia hicho kwa maana ya uwanja wa kuchezea na viwanja vya mazoezi, tunatarajia ndani ya siku 14 kama walivyotuahidi watatutumia ripoti," alisema Wambura.

Alisema majibu yanaweza kuwa mawili, kuridhika au kama kuna mapungufu basi watawaambia ili kuendelea kufanya marekebisho.

**"Kama kuna upungufu wameuona, watatuambia ni marekebisho ya kiasi gani yanahitajika, kwa hiyo tumefikia hapo hadi sasa na ikumbukwe kuwa michuano hii ya CHAN ni maandalizi ya Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), ambayo sisi ni wenyewe 2027," alisema Wambura.**

Nchi zote tatu za Tanzania, Kenya na Uganda, zimepewa wenyeji wa CHAN mwaka huu, ikiwa ni maandalizi ya Fainali za Mataifa ya Afrika 2027 iliyopewa jina la 'Pamoja AFCON.'

Kwa upande wa Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo nchini, Ally Mayay, alisema miongoni mwa viwanja vilivyokaguliwa ni uwanja uliopo nyuma ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, Uwanja wa Chuo cha Polisi Kurasini, pamoja na ule wa Gymkhana uliopo Posta.

"Baada ya kufika hapa walikagua viwanja vya mazoezi ambavyo vitaendana na hadhi ya CAF kila timu inatakiwa ifanye mazoezi kwenye uwanja unaoendana na uwanja wa mechi itakapochezwa, bahati nzuri Jeshi la Polisi limetupa ushirikiano mkubwa tuufanyie ukarabati," alisema Mayay.

Alisema kwa upande wa Uwanja wa Benjamin Mkapa, marekebisho yake yanaendelea ambapo kwa mujibu wa mkandarasi mpaka Agosti mwaka huu utakuwa umefikia asilimia 90.

"Walipofika hapa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, hawakuwa na wasiwasi kwa kuwa ni wenyeji na wameona maboresho yanayoendelea," alisema.



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbalo (kushoto), akimkabidhi Kombe la Mashindano ya Odo Ummy Cup, Nahodha wa timu ya Kiomoni FC, baada ya kuibuka mabingwa kwa kuifunga Nguvumali FC kwa mikwaju ya penalti 3-1 kwenye mchezo wa fainali uliopigwa Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga juzi. Kwa ubingwa huo, Kiomoni FC ilizawadiwa Sh. milioni tatu, pikipiki ya magurudumu matatu, ng'ombe, jezi seti pamoja na mpira. Kulia ni Mbunge wa Jimbo la Tanga Mjini (CCM), Ummy Mwalimu, ambaye ni Waziri wa Afya na kushoto ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga, Rajab Abdulrahman. **MPIGAPICHA WETU**

# KenGold haishikiki Ligi Championship

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Yanga ikiwa haishikiki kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, ikionekana kukaribia ubingwa, hali ni hivyo hivyo Ligi ya Championship kwa KenGold ambayo inaonekana hakuna wa kuizuia kupanda daraja, ilipoifumua Stand United mabao 2-0 juzi ikiwa ugenini.

Ikiwa kwenye Uwanja wa Kambarage Shinyanga, KenGold iliwaadhibu wenyeji wao idadi hiyo ya mabao na kufikisha pointi 56 kwa michezo 24 iliyochezwa, ikibakisha mechi sita tu kumaliza michezo yake 30 ya msimu huu.

Matokeo hayo yanaifanya kuwa huenda ikawa moja kati ya timu mbili zitakazopanda Ligi Kuu Tanzania Bara moja kwa moja kwa ajili ya msimu ujao bila kusubiri michezo ya 'play off.'

Wakati timu hiyo ikiwa karibu kukata tiketi ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao, vita kubwa ipo kwa Pamba FC, Biashara United, Mbeya Kwanza na TMA ambazo zinaonekana kuwania nafasi ya pili ya kupanda moja kwa moja, zote zikiwa zimecheza mechi 24 na kubakisha michezo sita.

Pamba FC ipo nafasi ya pili ikiwa na pointi 51, Biashara United nafasi ya tatu na pointi zake 50, Mbeya Kwanza inashika nafasi ya nne ikiwa na pointi 47 na TMA ikiwa nafasi ya tano ikimiliki pointi 45.

Timu za Ruvu Shooting na Pan African zipo kwenye hatari ya kushuka daraja ambapo huenda msimu ujao zikaenda kucheza Ligi Daraja la Pili 'First League' kama zisipofanya vizuri katika michezo yao sita iliyobaki kila moja.

Pan, inashika nafasi ya 15 ikiwa na pointi 15 na Ruvu Shooting timu ambayo ilishuka daraja msimu uliopita inaburuza mkia ikiwa na pointi 11.

**Pan, inashika nafasi ya 15 ikiwa na pointi 15 na Ruvu Shooting timu ambayo ilishuka daraja msimu uliopita inaburuza mkia ikiwa na pointi 11.**

# JKT Tanzania yapania kuibukia kwa Prisons leo

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha JKT Tanzania kikishuka dimbani leo kuwakabili Tanzania Prisons, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, George Mketo, amesema licha ya kushika nafasi ya pili kutoka mkiani mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara, wanaamini hawatashuka daraja na msimu ujao wataendelea kukipiga Ligi Kuu Tanzania Bara.

JKT Tanzania yenye pointi 19 baada ya kushuka dimbani mara 19, itaikaribisha Tanzania Prisons katika Uwanja wa Meja Jenerali Isamahyo, uliopo Mbweni Dar es Salaam, ambayo ipo nafasi ya sita na alama zake 27 ilizozikusanya katika michezo 20.

Kuelekea mchezo huo Mketo amesema wamefanya maandalizi mazuri ya kutafuta pointi tatu katika dimba la nyumbani kwao kutoka kwa mpinzani wao, Tanzania Prisons.

Alisema hawakufanya vizuri katika michezo ya nyuma, hivyo mechi ya leo ni muhimu kupata matokeo kwani wanahitaji pointi hizo ili kujiondoa kwenye nafasi ya chini ya msimamo.

"Hatujakata tamaa na tunaimani ya kubaki katika ligi kwa msimu ujao, ni kweli hatuna matokeo mazuri katika michezo ya nyuma, lakini ninaimani mechi ya leo ndiyo inaenda kututoa hapa tulipo kwa kusaka pointi tatu dhidi ya Tanzania Prisons.

"Ukiangalia mechi tumecheza 19 na tumevuna alama 19, ni wastani wa pointi moja kwa kila mechi, hatutaki kuona tunafanya makosa ya nyuma, tutahakikisha tunasaka pointi kila mechi tukianza na Prisons," alisema Mketo.

Naye Kocha wa Tanzania Prisons, Shabani Mtupa, alisema wamefanya maandalizi kulingana na ubora na udhaifu wa JKT Tanzania, muhimu kwao ni kusaka pointi baada ya kupoteza mbele ya Mtibwa Sugar.

"Hautakuwa mchezo rahisi, utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu hizo timu zote ni za taasisi kama Kulwa na Doto, kila mmoja anahitaji kupata pointi, JKT wanataka kujiondoa chini lakini sisi tunataka alama tatu ili kushika nafasi ya nne," alisema Mtupa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BRANTHWAITE SHABAHA UTD

KLABU ya Manchester United imemfanya mlinzi wa Everton na England chini ya umri wa miaka 21, Jarrad Branthwaite kuwa shabaha yao kuu ya uhamisho wa majira ya joto. ***(Star)***

### OLISE KUNG'OLEWA PALACE

WINGA wa Crystal Palace Mfaransa Michael Olise mwenye umri wa miaka 22, pia yuko juu kwenye orodha ya Manchester United ya majira ya joto. ***(Football Transfers)***

### GREAVES ATAKIWA EVERTON

EVERTON inamtaka beki wa Hull City, Jacob Greaves mwenye umri wa miaka 23, ambaye anatarajiwa kuhamia Ligi Kuu England msimu huu wa majira ya joto ikiwa klabu hiyo ya Championship itashindwa kupanda daraja. ***(Football Insider)***

### BRUNO RADA KWA CITY

MANCHESTER City inachunguza kumnunua kiungo wa kati wa Newcastle United, Mbrazil Bruno Guimaraes, mwenye umri wa miaka 26, ambaye ana kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 100 katika mkataba wake. ***(Football Transfers)***

### NETO AGOMBEWA SPURS

TOTTENHAM Hotspur imeungana na Manchester City, Liverpool, Newcastle United na Arsenal kwa matumaini ya kumsajili winga wa Ureno, Pedro Neto mwenye umri wa miaka 24, kutoka Wolves msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### AMPENDEKEZA AIT-NOURI

KOCHA anayeondoka Jurgen Klopp amependekeza Liverpool imsajili beki wa kushoto wa Algeria, Rayan Ait-Nouri kutoka Wolves, ingawa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, pia yuko kwenye rada za Manchester United. ***(TeamTalk)***

### PINTO AITAKA NEWCASTLE

MKURUGENZI wa zamani wa Michezo wa AS Roma, Tiago Pinto, ambaye alifanya kazi na kocha Jose Mourinho katika klabu hiyo ya Italia, amesema ana nia ya kumrithi Dan Ashworth anayejiunga na Manchester United kule Newcastle. ***(i Sport)***

### SANCHO HATAKI KURUDI

WINGA wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23, hana nia ya kurejea Manchester United baada ya muda wake wa mkopo katika Klabu ya Borussia Dortmund huku akimlaumu kocha Erik ten Hag kwa kuvuruga maisha yake ya soka. ***(Bild, via 90min)***

### MALEN KUMBADILI SANCHO

KLABU ya Dortmund ina nia ya kumbakisha Jadon Sancho na inaweza kutafuta makubaliano ya kubadilishana na Manchester United, ambayo yatamfanya mshambuliaji wa Uholanzi, Donyell Malen mwenye umri wa miaka 25, kuhamia pale Old Trafford. ***(Fichajes)***

### DORGELES ATAJWA CHELSEA

CHELSEA ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia kiungo wa kati wa FC Nordsjaelland ya Denmark, Mario Dorgeles, 19. ***(Tipsbladet)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CANCELO: NABAKI BARCA, SITAKI KURUDU MAN CITY

**BARCELONA,** Hispania

JOAO Cancelo amethibitisha kwamba, anatumaini kuona mkopo wake kutoka Manchester City kutua Barcelona unakuwa wa kudumu msimu huu wa majira ya joto.

**Cancelo amekaa msimu huu na Barca kwa mkataba ambao haujumuishi kipengele cha ununuzi, ingawa maofisa wa klabu hiyo wameweka wazi tangu kuanza kwa kampeni kwamba wanatarajia kupata mkataba wa kudumu mwishoni mwa msimu huu.**

Akizungumza na La Gazzetta dello Sport kabla ya mchezo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora kati ya Barcelona na Napoli, Cancelo aliweka wazi kuwa anataka klabu hizo mbili kuafikiana.

●●● Kwangu ni fahari kuvaa jezi hii, hakuna klabu nyingine nyingi ambazo naweza kwenda...

"Nimekuwa na bahati ya kucheza tu katika timu kubwa, ninajivunia sana safari yangu na kazi yangu kwa sababu hakuna mtu aliyewahi kunipa chochote," alisema.

"Sijui chochote kuhusu siku zijazo, lakini ningependa kubaki hapa. Nilikua nikiipenda sana Barca ya Ronaldinho, ndio aliyenifanya nipenda klabu hii, kwangu ni fahari kuvaa jezi hii. Na hakuna klabu nyingine nyingi ambapo mimi naweza kwenda."

Cancelo yuko chini ya mkataba na Man City hadi 2027, lakini kocha Pep Guardiola amekuwa akisisitiza kwamba atamruhusu mchezaji yeyote kuondoka ikiwa ataomba kuondoka.


Hivyo, mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ureno atapatikana kwa ajili ya kuuzwa msimu huu wa majira ya joto.

Hata hivyo, tatizo la Barcelona ni kwamba City hawajajiandaa kumpoteza Cancelo kwa uhamisho wa bure.

Gazeti la Mundo Deportivo hivi majuzi lilipendekeza kuwa wanaweza kudai pauni milioni 26 ambazo kwa kuzingatia masuala ya kifedha ya Barca, inaweza kuwa tatizo kubwa.

Wakala Jorge Mendes amepewa jukumu la kutafuta suluhu, huku Barca wakitumai kuwa uamuzi wa Cancelo kubakua Katalunya unaweza kuwasaidia kujadili punguzo.

# MOURINHO AFICHUA MIPANGO KURUDI KWENYE UKOCHA



**LONDON,** England

JOSE Mourinho amedai kuwa anatazamia kurejea katika ukocha, ingawa hataki kujichanganya na kutua sehemu ambayo sio sahihi kwake.

Mourinho kwa sasa hana kazi baada ya kutimuliwa AS Roma Januari baada ya kutupwa nje kwenye Coppa Italia na wapinzani wao, Lazio na kushika nafasi ya tisa kwenye jedwali la Serie A.

Giallorossi hao wamezaliwa upya chini ya uongozi wa gwiji wa klabu hiyo, Daniele De Rossi na wanawinda kwa dhati nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Mreno huyo amekuwa akihusishwa na majukumu mbalimbali tangu aondoke Roma na amekuwa akitajwa katika siku za hivi karibuni kwamba anaweza kurudi kwa mara ya tatu kule Chelsea. Mourinho alitembelea mashindano ya Formula 1 ya Saudi Arabia Grand Prix mwishoni mwa wiki na alizungumza na Sky Sports kuhusu mipango yake ya baadaye.

Alipoulizwa kama atarejea kwenye uongozi hivi karibuni, Mourinho alijibu: "Natumai hivyo. Nataka kurudi kwenye ukocha.

"Roma ilikuwa nzuri kwa sababu tulifanya fainali mbili za Ulaya ndani ya miaka miwili na ni ngumu katika klabu kufanya hivyo.

"Lakini sasa natakiwa kusubiri fursa sahihi. Nataka kufanya kazi kesho ikiwezekana, lakini sitaki kufanya uamuzi mbaya."

Mashabiki wa Chelsea waliimba jina la Mourinho wakati wa sare ya mabao 2-2 ugenini hivi majuzi dhidi ya Brentford, na pia kumpendelea mmiliki wa zamani Roman Abramovich. Pia waliimba dhidi ya Kocha Mkuu wa sasa, Mauricio Pochettino na Mwenyekiti, Todd Boehly.

Mourinho aliiongoza 'The Blues' kushinda mataji mawili mfululizo ya Ligi Kuu England na mataji manne ya nyumbani katika kipindi chake cha kwanza kama kocha pale Stamford Bridge kati ya 2004 na 2007.

Pia walitolewa nje ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika hatua ya nusu fainali mara mbili na Liverpool. Baada ya kuiongoza vyema Inter na Real Madrid, Mourinho alirejea Chelsea mwaka 2013. Alishinda taji lingine la Ligi Kuu na Kombe la Ligi kabla ya kutimuliwa Desemba 2015.

# Diaz aitosa Hispania, kuichezea Morocco

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Brahim Diaz, ameamua kuiwakilisha Morocco badala ya Hispania katika ngazi ya kimataifa kutokana na kukosekana kwa mawasiliano kati yake na Shirikisho la Soka la Hispania (RFEF), vyanzo vimethibitisha kwa ESPN.

Diaz mwenye umri wa miaka 24, alizaliwa mjini Malaga kwa mama Mhispania na baba Mmorocco. Amewakilisha Hispania katika ngazi mbalimbali za Timu ya Taifa ya Vijana na ana mechi moja kwa upande wa wakubwa, lakini Morocco imemshawishi kubadili nchi ya kuichezea kimataifa.

Kipaumbele cha Diaz kilikuwa wa kuichezea Hispania, kwani mshambulizi huyo wa zamani wa Manchester City alichezea timu ya wakubwa mnamo mwaka 2021 wakati mlipuko wa COVID-19 ulipolazimisha 'La Roja' hao kuchezesha timu yao ya vijana chini ya miaka 21 dhidi ya Lithuania. Diaz alifunga katika ushindi wa mabao 4-0 katika mchezo huo wa kirafiki.

Kwa kuwa mechi hiyo ilikuwa ya kirafiki, Diaz yuko huru kubadili nchi ya kuichezea kimataifa kutokana na sheria na kanuni za shirikisho la Mpira wa Miguu duniani (Fifa), kuruhusu hilo.

Na sasa ataitwa kwenye kikosi cha Morocco maarufu kama Simba wa Atlas kwa mara ya kwanza baadaye wiki hii kwa ajili ya mechi dhidi ya Angola na Mauritania baadaye mwezi huu. Vyanzo vilivyo karibu na Diaz viliiambia ESPN kuna kukatishwa tamaa na kushangazwa na namna RFEF walivyolishughulikia hilo.

Vyanzo hivyo vinaangazia msukumo wa kumshawishi chipukizi wa Barcelona, Lamine Yamal, ambaye pia alistahili kuichezea Morocco, lakini ameichagua Hispania baada ya RFEF kutuma maofisa wa ngazi za juu kukutana na Yamal.

Ingawa vyanzo vya RFEF vinasisitiza kuwa wamemtendea Diaz sawa na wachezaji wengine ambao walipata fursa ya kuwakilisha zaidi ya nchi moja, na kuongeza kuwa hawaelewi mabadiliko yake.

"Kila mtu ana uhuru wa kufanya maamuzi yake. Kwangu mimi kuna hatua tatu za kuitwa kwanza, pili unataka kuchezea timu ya taifa na tatu kocha akuchague," alisema kocha wa Hispania, Luis de la Fuente akiwaambia waandishi wa habari juzi.

# Nyota Man United fiti kuikabili Liverpool

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amefichua Rasmus Hojlund, Harry Maguire na Aaron Wan-Bissaka wanaweza kurejea baada ya kupona majeraha kwenye mechi yao ya Kombe la FA dhidi ya Liverpool Jumapili.

Msimu wa 'Mashetani Wekundu' hao umekumbwa na majeraha na magonjwa mbalimbali, huku Ten Hag akilalamika mara kwa mara kwamba wamevuruga maendeleo ya kikosi chake baada ya kampeni kali ya 2022/23.

Hata hivyo, huku kukiwa na mechi ngumu ya raundi ya sita ya Kombe la FA nyumbani dhidi ya wapinzani wao Liverpool, Mholanzi huyo amethibitisha kuwa nyota wake watatu wamerejea tena dimbani.

"Natumaini, wengine watarejea," alisema Ten Hag kuhusu wachezaji wake kwenye TalkSPORT.

"Aaron Wan-Bissaka alikuwa uwanjani kwenye mazoezi. Tunatarajia pia Harry Maguire kurejea kikosini wiki hii. Rasmus Hojlund ana matumaini makubwa atafanikiwa pia."

Mechi ya Jumapili na Liverpool inawakilisha nafasi ya mwisho kwa United kutwaa taji msimu huu, huku pia wakiwa tayari kuharibu ziara ya Jurgen Klopp ya kumuaga.

"Ni wazi. Ni mchezo mzuri kwetu na tunatazamia mchezo huo," aliongeza Ten Hag.

"Lakini Liverpool itakuwa sawa na pia kwa sababu itacheza kwao, pia ni mchezo muhimu sana.

"Tutapanga, tujiandae vizuri sana na tunapaswa kujiandaa kwa mchezo. Ni mchezo mkubwa."

United waliwabana Liverpool kwa sare ya bila kufungana kwenye Uwanja wa Anfield mwanzoni mwa msimu, lakini pia watakutana tena Old Trafford katika mechi ya Ligi Kuu England Aprili 7, mwaka huu.



# MANDONGA AJA NA 'JIWE LA MOTO' KUMVAA MAUGO

Na Shufaa Lyimo

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Karim Mandonga, amesema sasa anakuja na staili mpya ya 'jiwe la moto' kuelekea kwenye pambano lao la 'kuvunja upishi' dhidi ya Mada Maugo, watakalocheza Aprili mwaka huu mjini Morogoro.

Akizungumza na Nipashe jana, Mandonga alisema anaendelea kujifua kuhakikisha anamtwanga Maugo ndani ya raundi ya kwanza.

**“Sasa hivi nakuja na jiwe la moto, Maugo haniumizi kichwa ni bondia wa kawaida, nimepania kumpa kichapo kikubwa,” alisema Mandonga.**

Alisema kwa sasa anaendelea kufanya mazoezi yake Bonyokwa, Kimara nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, akiwa chini ya Kocha wake Mkuu, Said Kisopu, kabla ya kurudi mkoani Morogoro.

Bondia huyo aliwataka mashabiki wake wajitokeze kwa wingi siku hiyo wajionee burudani atakayowapa akiwa na lengo la kuzidi kuinua kiwango chake.

Alisema hana muda wa kuongea sana bali anataka kuonyesha vitendo akiwa ulingoni kwani anajiamini kwa kiasi kikubwa atamtwanga Maugo.

Aidha, aliwataka mabondia wachanga kuongeza juhudi katika mazoezi kwani mchezo wa ngumi kwa sasa unazidi kuitangaza Tanzania ndani na nje ya nchi.




Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania, Jenerali Jacob Mkunda (katikati), akikata utepe kuzindua hafla maalum ya kukabidhi mabasi kwa timu za jeshi hilo; JKT Queens, JKT Tanzania pamoja na Mashujaa FC, ambapo pia alizindua kamati ya uanzishwaji wa vituo vya michezo JWTZ. Hafla hiyo ilifanyika katika viwanja vya Gofu Lugalo, Dar es Salaam jana. Mabasi hayo yanauwezo wa kubeba abiria 55 kila moja. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

## Dodoma jiji hali si shwari

Na Adam Fungamwango

UONGOZI wa Dodoma Jiji FC, umesema hauridhishwi na mwenendo wa timu yao katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayoelekea ukingoni.

Ofisa Habari wa timu hiyo, Patrick Semindu, amesema hata wao viongozi hawafurahishwi na hali hiyo, lakini akiwataka mashabiki wa timu hiyo kuwa watulivu kwani changamoto zote zinafanyiwa kazi.

Jumamosi iliyopita, timu hiyo ilijikuta ikifungwa bao 1-0 dhidi ya Geita Gold mbele ya mashabiki wake, Uwanja wa Jamhuri, Morogoro.

“Nakiri kabisa kuwa kwa sasa mwenendo kwa upande wa matokeo si wa kuridhisha, tunajua hii inaumiza sana mashabiki wetu, lakini na sisi kama uongozi kitu hiki hakitufurahishi na tayari tumeanza mikakati maalum ya kuangalia mapungufu kwenye kikosi chetu kupitia kwa mwalimu,” alisema Ofisa Habari huyo.

Aliwataka mashabiki wa timu hiyo licha ya changamoto hiyo kuendelea kuiunga mkono timu yao kwani wameahidi kurekebisha hali hiyo, huku malengo yao ya kuwa moja ya timu nne za juu yakiwa pale pale.

“Mwalimu ameahidi kuyafanyia kazi mapungufu yote mara moja, tuna muda wa kufanya, kwa sababu mechi yetu inayofuata tutacheza Aprili 14 dhidi ya Kagera Sugar.

“Tunawaomba mashabiki wa Dodoma Jiji watulie, waendelee kutuunga mkono ili tutimize azma yetu ya kumaliza kwenye nafasi nne za juu, malengo yetu yapo pale pale,” alisema Semindu.

Dodoma Jiji inashika nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 23, ikicheza mechi 20, ikishinda sita, sare mitano na ikipoteza tisa.



Kocha wa Dodoma Jiji, Francis Baraza.

## *Simba kwa Al Ahly CAF, Yanga kwa Mamelodi*

INATOKA UKURASA 24

kama ilivyokuja, na kwa sababu klabu yao inataka kuwa kubwa basi ni lazima icheze na kuzishinda timu kubwa.

“Tumeipokea vizuri na haikuwa na namna kwa sababu timu zote zilizoingia hatua hiyo ni ngumu na nzuri, sasa tunapoelekea kwenye mechi ya robo fainali, kuna vitu kadhaa inabidi vifanyike.

Kwanza wachezaji wetu wanatakiwa wajiamini, kujiamini ni jambo moja, pili ni kupambana, mwisho ni mashabiki wetu watupe sapoti ili tuweze kupambana na timu hiyo ngumu na tusonge mbele,” alisema kiongozi huyo.

Timu zote za Tanzania zitaanzia nyumbani kati ya Machi 29 hadi 30, na kwenda kumalizia ugenini kati ya Aprili 5 hadi 6, mwaka huu.

Kwa mujibu wa droo hiyo, mshindi kati ya Simba na Al Ahly anatarajiwa kucheza na mshindi kati ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo itakayokumbana na Petro de Luanda ya Angola, na kama Yanga itashinda mechi dhidi ya Mamelodi itakuwa na kibarua kingine hatua ya nusu fainali dhidi ya Esperance ya Tunisia au Asec Mimosas ya Ivory Coast.

Msimu huu, Simba iliingia hatua hiyo ikishika nafasi ya pili kutoka Kundi B na pointi zake tisa, ikiwa ni mara ya nne, huku Yanga ikitinga mara ya kwanza ikiwa ya pili kwenye Kundi D, ikimaliza na pointi nane.

## Azam FC yaipeleka Yanga kwa Mkapa

INATOKA UKURASA 24

Yanga.

Alisema wamefanikiwa na juzi wamepokea majibu kutoka serikalini kuwa wanaruhusiwa kutumia uwanja huo kama wa nyumbani katika michezo hiyo na wataanza dhidi ya Yanga.



“Kikubwa tumekubaliwa kutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa, tutaanza kutumia uwanja huo katika mechi yetu ijayo dhidi ya Yanga, Machi 16, mwaka huu, pamoja na Simba ambao tutacheza nao mzunguko wa pili.


“Kikosi chetu chini ya Kocha Youssouph Dabo, kinaendelea kuwajenga wachezaji kimbinu na kiufundi na kisaikolojia kuhakikisha tunafanikiwa kutumia uwanja huo vizuri na kuvuna pointi muhimu katika michezo hiyo miwili,” alisema Zaka za Zakazi.

Zaka (pichani) alisema lengo lao kubwa ni kutafuta pointi tatu na kuona timu yao inafikia malengo yao kwa sababu wanaangalia zaidi mikakati yao na hawataingia katika vita vya mbio za ubingwa wa Ligi Kuu kwa sasa.

**Michezo**

Jumatano Machi 13, 2024

Nipashe



Mourinho afichua kurudia ukocha UKURASA 21




# *Simba na Al Ahly CAF, Yanga kwa Mamelodi*

- Makocha wasema acheni waje tunawafahamu vizuri, wataja mikakati ya ushindi...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI miamba ya soka na wawakilishi wa nchi kwenye ngazi ya klabu katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba na Yanga zikipangwa kukutana na Al Ahly ya Misri na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kwenye hatua ya robo fainali, makocha wa timu hizo wamesema "acheni waje tunawafahamu vizuri".

**Katika droo ya michuano hiyo iliyochezeshwa jijini Cairo, Misri jana alasiri Simba wamepangwa kucheza na Mabingwa Watetezi, Al Ahly, huku Yanga ikijikuta ikiangukia kwa Mamelodi Sundowns.**

Simba imepangwa kucheza na Al Ahly, ikiwa ni miezi mitano tu baada ya kukutana kwenye michuano ya African Football League, AFL.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Oktoba 21, mwaka jana, timu hizo zilitoka sare mabao 2-2 na ziliporudiana tena, Oktoba 24, zikatoka tena sare ya bao 1-1 na Simba kutolewa kwa kanuni ya bao la ugenini.

Timu hizo pia zilikuwa pamoja kwenye hatua za makundi msimu wa 2018/19 zikiwa Kundi D na zote zikasonga mbele hatua ya robo fainali, Al Ahly ikiongoza kundi, Simba ikifungwa mabao 5-0 ugenini na kushinda bao 1-0 nyumbani.

Zilikutana tena mara mbili hatua ya makundi msimu wa 2020/21, kila timu ikishinda bao 1-0 nyumbani, zote mbili zikisonga mbele, Simba ikiongoza kundi hilo.

Baada ya droo hiyo, Kocha Msaidizi wa Simba, Seleman Matola, alisema katika hatua hiyo hakuna kukwepa yeyote lazima watakutana naye na wanaenda kucheza kwa mara nyingine na Al Ahly.

Alisema hakuna mchezaji, benchi la ufundi hata viongozi wa Simba ambaye haifahamu Al Ahly, kwani wameshakutana nayo mara kadhaa na kufanikiwa kupata matokeo mazuri.

"Tukumbuke hivi karibuni tulikutana naye katika African Football League (AFL), kati ya timu nane tunaenda kutolewa kwao na bahati haikuwa kwetu. Sasa ni wakati wa kuchanga karata zetu vizuri kwenda kupambana naye.

"Hatuna presha juu ya mechi ya nyumbani kikubwa tunafanya maandalizi kwa ajili ya kuhakikisha tunafanikiwa kusonga mbele kwa kujiweka imara kupambana na Al Ahly ambaye tunamfahamu vizuri akiwa ugenini na nyumbani," alisema Matola.

Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga, itakuwa ni mara ya kwanza kukutana na Mamelodi Sundowns katika historia ya timu hiyo.

Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema wanakutana na timu bora Afrika na anaifahamu kwa sababu aliwahi kukaa Afrika Kusini na anajua misingi ya mpinzani wake huyo jambo ambalo ataitumia kupata matokeo mazuri.

"Katika hatua hii hakuna mdogo wala mnyonge hakuna aliyefika kwa bahati, bali alipambana na kufika hapa, tunamfahamu Mamelodi Sundowns, si timu ndogo tuko tayari kwa mchezo wa hatua ya robo," alisema kocha huyo raia wa Argentina.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Yanga, Andre Mtine, alisema wameipokea vizuru droo

INAENDELEA UKURASA 23

## Azam FC yaipeleka Yanga kwa Mkapa

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC umethibitisha kukubaliwa ombi lao na serikali kuutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kama uwanja wa nyumbani katika michezo yao miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara watakapocheza na Yanga na Simba.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Zakaria Thabit 'Zaka za Kazi', alisema walipeleka barua ya maombi serikalini kwa ajili ya kuomba kutumia Uwanja wa Mkapa katika michezo yao mikubwa miwili ya Simba na

INAENDELEA UKURASA 23



9 770856 541002 >